Oktoba – Desemba 2018

www.ccog.org

# Unabii wa Habari za BIBLIA




## Krismasi?
Siyo yangu

## Amri ya Kwanza
Je, Unampenda Mungu jinsi Unapaswa kumpenda?

# Dhiki Kuu na Wakati Mwisho wa Watu wa Mataifa


# UNABII WA HABARI ZA BIBLIA



4



8



14


19

## Katika Makala hii:


2 **Kutoka kwa Mhariri: Krismasi?** Siyo yangu.

4 **Amri ya Kwanza** Je, Unampenda Mungu jinsi Unapaswa kumpenda?

8 **Jisomee Kozi ya Biblia Somo la 14b: Je, Wanadamu ni nani?** Mungu anasemaje kuhusu wanadamu?

14 **Ni Injili Gani Yesu Alihubiri?** Je, Yesu alikuja duniani kuhubiri kuhusu nafsi yake au kuna ujumbe mwingine alihubiri ambao wengi wanakosa?

19 **Dhiki Kuu na Wakati wa Mwisho wa watu wa Mataifa** Dhiki Kuu inakuja kwa hivyo usitosheke sana kiasi cha kufikiri kwamba haitakufikia.

**Jalada la Nyuma:Intaneti na Redio** Hii inaonyesha watu mahali pa kupata ujumbe wa Kanisa la Mungu *Linaloendelea*.

**Kuhusu Jalada la Mbele:** James Erwin Estoque anaweka hizi pamoja akitumia sanaa ya tarakilishi ya kutunga picha.



**Unabii wa Habari za Biblia inchapishwa na Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG) 1036 W. Grande Ave. , Grover Beach, CA 93433 https://www. ccog. org**



**© 2018 Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG).**
**Imechapishwa Marekani. Haki zote zimehifadhiwa.**

Kunakili makala yote ama sehemu yake pasipo ruhusa ya kimaandishi toka kwa mmiliki hairuhusiwi. Tunaheshimu haki zako hivyo hatutoi, kuuza ama kukodisha orodha ya mawasiliano yetu. Endapo haungependa kuendelea kuupokea gazeti hili, wasiliana na afisi yetu ya Grover Beach. Maandiko yamenukuriwa toka New King James version © Thomas Nelson, Inc, Publishers, used by permission isipokuwa pale tu tumeelekezwa vinginevyo.


Unabii wa Habari za Biblia HUWEZESHWA KWA MICHANGO YENU.


**Mhariri Mkuu: Bob Thiel**

**Makala/Mhariri Msaidizi: Joyce Thiel**

**Mashahihisho: John Hickey**
**SBC Course Assister: Shirley Gestro.**

**Iliyoundwa na:**
James Erwin EStoque


Picha: Picha zote zimetokana na familia ya Thiel ama na vyanzo vya mitandao ya kijamii kama vile Wikipedia au picha za tarakilishi na za serikali fulani (ikiwa chanzo hakikutajwa, itakuwa ni kwa sababu inaaminika kwamba chanzo husika kiliachia piacha iwe matumizi ya umma pasipo masharti yo yote).

## KUTOKA KWA MHARIRI MKUU: BOB THIEL



# KRISMASI:

## Siyo Yangu.

Wengi wanaokiri kuwa Wakristo wanasherekea Krismasi. Mara nyingi inaadhimishwa tarehe 25 Desemba kwa wale wanaoishi sehemu ya Magharibi, ilhali ni tarehe 7 Januari kwa wale walioko Mashariki. Wale wanaoadhimisha siku hiyo wanadai kwamba wanasherekea kuzaliwa kwa Yesu.

Biblia yenyewe haijaidhinisha sherehe ya siku za kuzaliwa, pamoja na hata kuzaliwa kwa Yesu. Kanisa la awali la Rumi halikusherekea Krismasi na hata siku yo yote ya kuzaliwa kwa mtu. Sherehe ya kuzaliwa kwa mtu ilikataliwa hadi mwisho wa karne ya 3 na Arnobia katika kitabu chake (Dhidi ya Makafiri, Kitabu cha I, Sura ya 64).

Wakristo wa awali hawakusherekea Krismasi.

Zaidi ya hayo, Tertulia (aliyedaiwa kuwa ''baba ya thiolojia ya Kilatini, '') alionya kwamba kushiriki katika sherehe za majira ya baridi na kununua shada la maua pamoja na kupeana zawadi kunafanya mtu kushiriki katika kuabudu miungu ya kipagani. Katika kipindi chake, kulikuweko na sherehe iliyokuwa ikiitwa Sartunalia ambayo ilikuwa ikisherekewa na makafiri mnamo mwisho wa Desemba.

Tertulia alikana sherehe za majira ya baridi, kama vile Saturnalia(kutoka kwa mungu wa kipagani iliyoitwa maridhawa) ambayo iligeuka kuwa Krismasi kama vile alivyoandika:

> Minervalia kama vile Minerva, Sartunalia kama vile Zohali; Zohali ambayo lazima watu washerekee hata na watumwa wachanga kwa wakati wa sikukuu ya Sartunalia. Zawadi za mwaka mpya pia lazima zitolowe na Septimontia kuadhimishwa, na uwepo wote wa sherehe ya katikati ya majira ya baridi na sikukuu ya jamaa lazima ifanywe, shule lazima zing'arishwe na shada la maua, na aina za dhabihu zifanywe; shule zinatukuzwa katika sikukuu hizo. Kitendo kama hicho pia kinafanywa katika siku ya sanamu ya kusherekea siku ya kuzaliwa; kila pambo la Shetani linavaliwa kila mara. Ni nani atakayedhani kwamba vitu hivi vinasaidia Mkristo mhudumu, isipokuwa ni mtu ambaye atafikiri kadhalika kwa mtu ambaye sio mwalimu? (Tertullian. On Idolatry, Chapter X).

Wakati huo wa Tertulia, Maaskofu wa Rumi walioitwa Zefirina (199-217) na Kalisto (217-222) walikuwa na sifa ya ulegevu na ufisadi (na hilo liliakikishwa na watakatifu wa Rumi kama vile Hipolita). (Hippolytus. Refutation of Al Heresies, Book IX, Chapter VI) na wakaruhusu ulegevu huo wa kipagani, n. k.

Saturnalia ya Kirumi na mungu mke anayeitwa mithra wa Uajemi zenyewe zilitengenezwa na dini ya awali ya pagani-ile ya zamani ya Kibabeli ambayo ni dhehebu la siri. Wababeli wa zamani walisherekea kuzaliwa tena kwa Nimrodi kama Tammuzi kwa kuabudu mti wa kijani kibichi. Biblia inalaani ibada ya kuhusisha mti wa kijani kibichi (Kumbukumbu 12:2-3; Yeremia 3:13; 10:2-6).

Wababeli pia walisherekea kuzaliwa upya wa jua katika majira ya baridi. Tarehe 25 Desemba ndiyo ilichaguliwa kama siku ya kuzaliwa kwake Yesu, kwa sababu Saturnalia na ibada ya miungu mingine wa jua ilifanyika wakati huo wa mwaka:

> Mnamo 354 B. K. , Askofu Liberia wa Rumi aliamrisha watu kusherekea tarehe 25 Desemba. Alichagua tarehe hii kwa sababu watu wa Rumi tayari walikuwa wakiadhimisha tarehe hiyo kama Sikukuu ya Zohali, wakisherekea kuzaliwa kwake jua. (Sechrist EH. Chrismas. World Book Encyclopedia, Volume 3. Field Enterprises Educational Corporation, Chicago, 1966, pp. 408-417)

> Mithra Helio ni mungu mmoja...Jumapili iliadhimishwa kama siku takatifu ya Mithra na kila tarehe kumi na sita ya kila mwezi ilikuwa siku takatifu kwa Helio kama mpatanishi. Tarehe 25

> Desemba iliadhimishwa kama siku ya kuzaliwa kwake, yaani kuzaliwa kwa natalisinvicti, kuzaliwa tena kwa jua ya majira ya baridi, isiyoshindwa na ukali wa majira. (Arendzen J. Mithraism. The Catholic Encyclopedia, Volume X. Nihil Obstat, October 1, 1911).

Miaka michache kabla Liberia  hajaiweka hiyo siku kuwa rasmi, Mfalme Konstantino alikuwa mfuasi wa mungu wa jua anayeitwa Mithra. Mithra ilijulikana kuwa ni jua isiyoshindwa na ilizaliwa kutoka kwenye mwamba chini ya pango. Pengine kwa sababu hiyo, mamake Helena aliamini kwamba Yesu alizaliwa chini ya shimo la mwamba.

Rumi sasa inafundisha vilevile (na mwandishi huyu ameona ''kuzaliwa kwa Yesu'' kukionyeshwa mara nyingi sana Jijini Vatikani), lakini katika karne ya tatu mmoja wa wasaidizi, Komodiana, alilaani mungu wa mwamba:

> Yule asiyeshindwa alizaliwa kutoka kwenye mwamba, ikiwa akizingatiwa kuwa mungu. Sasa twambie, kwa njia nyingine, ni nani aliye wa kwanza kati ya hawa wawili. Mwamba ameushinda mungu:basi muumbaji wa mwamba anafaa atafutiwe. Zaidi ya hayo, bado anaonyeshwa kama mwizi; hata hivyo, ikiwa alikuwa mungu, bila shaka hakuishi kwa uwizi. Kwa ukweli alikuwa wa dunia, na alikuwa na tabia ya kuogofya. Na aligeuza fahali wa watu wengine kuingia katika mapango yake; kama vile Kakusi, yule mwana wa Vulkani. (Commodianus. On Christian Discipline)

Yesu hakuzaliwa kutoka kwenye mwamba, hata hivyo kuzaliwa kwake sasa kunaonyeshwa hivyo. Pia sio ukweli kufundisha kwamba alizaliwa tarehe 25 Desemba. Wasomi wanagundua kwamba wachungaji hawangekuwa nje malishoni (kama vile Biblia inaonyesha katika Luka 2:8) tarehe 25 Desemba na kwamba kuhesabu watu unaotajwa katika (Luka 2:1-5) ''haingefanyika wakati wa majira ya baridi'' (Chrismas. The Catholic Encyclopedia, 1908).

Matendo mengi na desturi zinazoambatana na Krismasi zinatoka kwa upagani kama vile wasomi kamili wanavyosema. Mitume wa Yesu na wafuasi wa awali hawakuadhimisha Krismasi.

## Mfundo wa Sikukuu za Kipagani

Wakati Biblia haikatai sikukuu za serikali (kama vile ''sikukuu ya madaraka''), watakatifu wa awali hawakuwaombea watakatifu waliokufa ama kuadhimisha kitu chochote kilichoitwa Krismasi.

Baadhi ya matendo ya kipagani yalibadilika, lakini mfundo wa sikukuu za kipepo bado si za Wakristo, na hata si zile sikukuu ambazo Yesu na wanafunzi wake waliadhimisha. Sikukuu nyingi ambazo watu wanaadhimisha zilitoka kwa upagani na hata zina uhusiano na dini ya siri ya Babeli. Wakati Mungu alituma Nehemia kuwasaidia wana wa Israeli ambao walishawishika na Babeli, tazama vile alivyofanya Nehemia:

> 30 Hivyo nikawatakasa na kila kitu kigeni. (Nehemia 13:30)

Agano Jipya linaonya kuhusu imani potofu ya '' Siri ya Babeli Mkuu'' (Ufunuo 17:5). Kumbuka Biblia inafundisha jinsi watu wa Mungu wanapaswa kufanya kuhusu ''Babeli Mkuu:''

> 4 ...Tokeni kwake, enyi watu wangu, msishiriki dhambi zake, wala msipokee mapigo yake. (Ufunuo 18:4)

Wakristo wanapaswa kuepukana na majaribu na dhambi (1 Wakorintho 6:18; 2 Timotheo 2:22), siyo kuambatana nayo na kuimarisha. Hawapaswi kuchanganya matendo ya pagani na ibada ya Mungu wa kweli (1 Wakorintho 10:19-21; 2 Wakorintho 6:14-18), na hata mapokeo ya watu (Mathayo 15:3-9).

Yesu alifundisha:

> 23 Lakini saa inakuja, nayo sasa ipo, ambao waabuduo halisi watamwabudu Baba katika roho na kweli. Kwa maana Baba awatafuta watu kama hao wamwabudu. 24 Mungu ni Roho, nao wamwabuduo yeye imewapasa kumwabudu katika roho na kweli. (Yohana 4:23-24)

Ukweli ni kwamba Krismasi siyo sikukuu ya Biblia, hata haikuwa sehemu ya imani ya awali, inatokana na mivuto ya kipagani, kwa hivyo Yesu hakuzaliwa katika tarehe hizo mbili ambazo zinaadhimishwa.

Jitahidi kuabudu Mungu wa ukweli-kuabudu Mungu wa ukweli siyo kuadhimisha Krismasi.

# AMRI ya KWANZA




## Na Bob Thiel

Je, maisha ya mwanadamu yanapaswa kuyategemea vitu vya mwili?

Hakika, wengi katika ulimwengu wanaishi kana kwamba maisha lazima yategemee vitu vya kimwili. Ndiyo, watu wana ibada na mapokeo yao. Na wengi wanaenda kanisani kusali.

Lakini ukichunguza vizuri, utapata kwamba Mungu sio wa muhimu kwao.

Ijapokuwa kwa Wakristo halisi, hili halifai kufanyika. Yesu alisema:

> 31 Msisumbuke, basi, mkisema, Tule nini? Au tunywe nini? Au tuvae nini? 32 Kwa maana hayo yote Mataifa huyatafuta; kwa sababu Baba yenu wa mbinguni anajua ya kuwa mnahitaji hayo yote. 33 Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa. (Mathayo 6:31-33)

Je, unaweka Mungu mbele kwanza?

Miongo mingi iliopita, nakumbuka mtu mmoja akiniambia kwamba Mungu hapaswi kuingia katika kazi yake. Alikuwa akidai kuwa ni Mkristo wa aina fulani. Hakuamini katika kumtafuta ufalme wa Mungu kwanza na haki yake, ili azidishiwe yote.

Yafuatayo ni Amri ya kwanza kutoka kwa Kitabu cha Kutoka:

> 2 Mimi ni BWANA, Mungu wako, niliyekutoa katika nchi ya Misri, katika nyumba ya utumwa.
> 3 Usiwe na miungu mingine ila mimi. (Kutoka 20:2-3).

Kwa sababu ya kumbukumbu ambalo linaonyesha kwamba Mungu aliwatoa wana wa Israeli kutoka Misri, wengi wamesema kwamba amri hii, na hata amri zingine, zilikuwa za wana wa Israeli peke yake.
Hata hivyo, mtazamo huo unakosa uhakika kwamba maelezo ya amri hii yalikuwepo kabla ya wana wa Israeli na hata baada ya Yesu kufufuliwa. Pia unakosa ukweli kwamba Biblia inaongea kuhusu Misri ya kiroho (Ufunuo 11:8).

Zaidi ya hayo, chunguza ikiwa umetoka kwa njia za uongo na mapokeo ya ulimwengu huu na ikiwa umetubu kutoka kwa tamaa na dhambi zako. Sote twapaswa kutoka kwa Misri ya kiroho.

Kumbuka baadhi ya maneno Mungu alimwambia Ibrahimu:

> 7 Kisha akamwambia, Mimi ni BWANA, niliyekuleta kutoka Uru wa Wakaldayo nikupe nchi hii ili uirithi (Mwanzo 15:7).
>
> 1 Mimi ni Mungu Mwenyezi, uende mbele yangu, ukawe mkamilifu (Mwanzo 17:1).

Biblia pia inasema:

> 5 Kwa sababu Ibrahimu alisikia sauti yangu, akahifadhi maagizo yangu, na amri zangu, na hukumu zangu, na sheria zangu. (Mwanzo 26:5).

Neno la Kiebrania lililotafsiriwa 'amri' hapa, mitswoyaay, pia limetajwa katika Kutoka 20:6 wakati Amri Kumi ziliorodheshwa.

Fungu hili katika Mwanzo linaonyesha kwamba Ibrahimu alitii na kujua alichotarajia Mungu. Na hii ilikuwa karne nyingi kabla ya Amri Kumi kutolewa kwenye Mlima wa Sinai.

> Wakristo pia wanashauriwa kwamba wawe watiifu (1 Petro 1:13-14).

## Je, Adamu na Hawa Walifanyaje?

> Mungu ndiye tunapaswa kumtii (Matendo 5:32).

Je, wagundua kwamba huo ni ufafanuzi wa Mungu? Ye yote unayemtii sana ndiye mungu wako. Kile unachokitumia ndicho kinaweza kuwa mungu

wako. Linaweza kuwa gari lako. Pengine ni sanamu. Pengine ni mwajiri wako ama familia yako. Chochote unachokitumia, hicho ndicho mungu wako ikiwa umeitii na kutomtii Mungu wa Biblia (Matendo 5:29).

> 16 Hamjui ya kuwa kwake yeye ambaye mnajitoa nafsi zenu kuwa watumwa wake katika kumtii, mmekuwa watumwa wake yule mnayemtii, kwamba ni utumishi wa dhambi uletao mauti, au kwamba ni utumishi wa utii uletao haki. (Warumi 6:16)

Adamu na Hawa walikuwa na mungu badala ya Mungu wa ukweli. Adamu na Hawa walikiuka amri ya kwanza. Hawa alitii sauti ya Joka (Mwanzo 3:13) na Adamu akaitii sauti ya Hawa (Mwanzo 3:17). Yoeli alifundisha:

> 12 Lakini hata sasa, asema BWANA, nirudieni mimi kwa mioyo yenu yote, na kwa kufunga, na kwa kulia, na kwa kuombolea. (Yoeli 2:12)

Mungu mara nyingi anahitaji kujitoa kamili.

## Amri Kuu

Amri kuu ni ipi? Yesu aliuliza swali hilo:

> 35 Mmoja wao, mwana-sheria, akamwuliza, akimjaribu; 36 Mwalimu, katika torati ni amri ipi iliyo kuu?37 Akamwambia, Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote. (Mathayo 22:35-37)

Watu wengi wanasema kwamba wanampenda Mungu, lakini Mungu sio halisi kwao. Wameweka vipaumbele vingine badala ya Kumtii Mungu.

Kumbuka vile Yoshua alivyonena:

> 14 Basi sasa mcheni BWANA, mkamtumikie kwa unyofu wa moyo na kwa kweli; na kuiweka mbali miungu ambayo baba zenu waliitumikia ng'ambo ya Mto, na huko Misri; mkamtumikie yeye BWANA. 15 Nanyi kama mkiona ni vibaya kumtumikia BWANA, chagueni hivi leo mtakayemtumikia; kwamba ni miungu ile ambayo baba zenu waliitumikia ng'ambo ya Mto, au kwamba ni miungu ya Waamori ambao mnakaa katika nchi yao; lakini mimi na nyumba yangu tutamtumikia BWANA. (Yoshua 24:14-15)

Je, Wakristo wanaamini kweli kwamba wanapaswa kuitumikia miungu wa uongo?

Hata hivyo, ijapokuwa Yesu alirejelea amri ya kwanza kama amri kuu, amri hii ndiyo inakiukwa sana.

Biblia inafundisha hivi:

> 5 Mtumaini BWANA kwa moyo wako wote, Wala usitegemee akili zako mwenyewe. 6 Katika njia zako zote mkiri yeye, Naye atanyoosha mapito yako. (Mithali 3:5-6)

Ijapokuwa, wengi hawatafanya hivyo. Badala yake, wengi wana hekima machoni pao na wanajiamini kwa akili zao. Biblia inaonya:

> 7 Usiwe mwenye hekima machoni pako; Mche BWANA, ukajiepushe na uovu. (Mithali 3:7)

Wale wanaotegemea hekima yao hawaamini Mungu na wanakiuka amri ya kwanza.

Wakristo wanapaswa kuomba kwamba mapenzi ya MUNGU yatendeke (Mathayo 6:10) na wawe na mtizamo wa Yesu ya ''si mapenzi yangu bali yako yatendeke'' (Luka 22:42).

Kama ilivyokuwa wakati wa Yesu, wengi wanakubali ''mapokeo ya wanadamu'' ambayo yanabatilisha kujitolea kwa kuitii amri ya Mungu (Mathayo 15:3-9) na hawatahatarisha kufukuzwa nje ya makanisa yanayolegeza ukweli kwa sababu ''walipenda utukufu wa wanadamu kuliko utukufu wa Mungu'' (Yohana 12:43).

Ikiwa watu watatunza amri ya kwanza, haungekuwepo na ugaidi. Hakungekuwa na kuzaa usiostahili. Hakungekuwa na magonjwa ya zinaa. Hakungekuwa na mauaji. Hakungekuwa na uwizi. Wanasiasa wangesema ukweli. Ulimwengu ungekuwa mahali pazuri.

Amri ya kwanza ni muhimu, na hakika kama vile ilivyo. Utiifu unaweza kuuleta wingi na amani. Jamii zingebadilika na amani ya kiroho ingetawala.
Wakati Shetani angejaribu kuwashawishi watu katika

nyakati hizi (Waefeso 2:2), watu wangefuata himizo la Yakobo:

> 7 Basi mtiini Mungu. Mpingeni Shetani, naye atawakimbia. 8 Mkaribieni Mungu, naye atawakaribia ninyi. (Yakobo 4:7-8)

Ulimwengu ungekuwa mahali pazuri ikiwa watu wangeitii amri ya kwanza.

## Kwa Nini Umpende Mungu?

Kwa nini unapaswa kumpenda Mungu? Kwa sababu:

> 17 Kila kitolewacho kilicho chema na kilicho kamili, hutoka juu, hushuka kutoka kwa Baba wa mianga, ambaye kwake hakuna kubadilika, wala kivuli cha kugeukageuka. 18 Kwa mapenzi yake mwenyewe alituzaa kwa neno la kweli, kusudi tuwe kama mazao ya kwanza katika viumbe vyake vyote. (Yakobo 1:17-18)

Kila zawadi njema inatoka kwa Mungu. Zaidi ya hayo, Yesu ndiye alikuwa ''mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi'' (Warumi 8:29). Mungu ana mpango nasi ya kututukuza kama vile alivyomtukuza Yesu (Yohana 17:22).

Mungu anapanga kuweka ulimwengu chini ya mamlaka ya watoto wake watakaofufuliwa (Waebrania 2:5-10)! Zaidi ya hayo, pia kumbuka:

> 19 Sisi twapenda kwa maana yeye alitupenda sisi kwanza. (1 Yohana 4:19)

> 8 Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi. 9 Basi zaidi sana tukiisha kuhesabiwa haki katika damu yake, tutaokolewa na ghadhabu kwa yeye. (Warumi 5:8-9)

Licha ya shida uliyo nayo, unazo ahadi kuu za ajabu:

> 28 Nasi twajua ya kuwa katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema, yaani, wale walioitwa kwa kusudi lake. (Warumi 8:28)

> 6...yeye aliyeanza kazi njema mioyoni mwenu ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu. (Wafilipi 1:16)

Mungu alituumba. Vitu vyote vizuri vyatoka kwa Mungu. Licha ya dhambi zetu, alituma Yesu atufie (Yohana 3:16). Ikiwa twampenda Mungu mambo yote yatatuendea mema, kwa hivyo Mungu atakuwa mwaminifu hadi wakati wa Yesu na atatukuza. Tunayo mengi ya kumpendea Mungu!

## Ujasiri wa Uongo

Tunapaswa tutegemee Mungu wa Biblia. Ijapokuwa, wengi katika historia wametegemea falaki, uchawi na wale wanaoongea na mapepo (Isaya 47:13-15). Hicho si kitu ambacho watu wa Mungu wanafaa wafanye:

> 19 tena usije ukainua macho yako hata mbinguni, na ulionapo jua, na mwezi, na nyota, jeshi la mbinguni lote pia, ukashawishwa na kuviabudu, na kuvitumikia, ambavyo BWANA, Mungu wako amewagawanyia watu wote chini ya mbingu zote. (Kumbukumbu 4:19)

> 10 Asionekane kwako mtu ampitishaye mwanawe au binti yake kati ya moto, wala asionekane mtu atazamaye bao, wala mtu atazamaye nyakati mbaya, wala mwenye kubashiri, wala msihiri, 11 wala mtu alogaye kwa kupiga mafundo, wala mtu apandishaye pepo, wala mchawi, wala mtu aombaye wafu. 12 Kwa maana mtu atendaye hayo ni chukizo kwa BWANA; kasha ni kwa sababu ya hayo BWANA, Mungu wako, anawafukuza mbele yako. 13 Uwe mkamilifu kwa BWANA, Mungu wako. 14 Maana mataifa haya utakaowamiliki huwasikiliza wanaoshika nyakati mbaya na kutazama bao; bali wewe BWANA, Mungu wako, hakukupa ruhusa kutenda hayo. (Kumbukumbu 18:10-14)

Wakristo hawasomi buruji, n. k. Tunatazama Biblia (Isaya 8:10; 66:5). Wakristo hawafuati ''hadithi zilizotungwa kwa werevu'' (2 Petro 1:16).

## Amri ya Kwanza Kabla ya Sinai, kutoka kwa Yesu, na Baada ya Kifo cha Yesu

> ''Mimi ni BWANA, niliyekuleta kutoka Uru''

(Mwanzo 15:7); ''Mimi ni Mungu Mwenyezi, uende mbele yangu, ukawe mkamilifu'' (Mwanzo 17:1); ''Mimi ni Mungu wa baba yako, Mungu wa Ibrahimu, Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo. '' (Kutoka 3:6). ''Ondoeni miungu migeni iliyoko kwenu, mjisafishe'' (Mwanzo 35:2). ''nami nitafanya hukumu juu ya miungu yote ya Misri; Mimi ndimi BWANA'' (Kutoka 12:12). ''Sasa najua ya kuwa BWANA ni mkuu kuliko miungu yote; naam, katika jambo hilo walilowatenda kwa unyeti'' (Kutoka 18:11). ''Hilo nalo lingekuwa uovu wa kuadhibiwa na waamuzi, Kwani ningemwambia uogo Mungu aliye juu'' (Ayubu 31:28). ''Ndipo Ayubu akamjibu BWANA, na kusema. Najua ya kuwa waweza kufanya mambo yote, Na ya kuwa makusudi yako hayawezi kuzuilika'' (Ayubu 42:1-2).

Yesu alifundisha na kupanua amri ya kwanza:

''Msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu yeye peke yake'' (Mathayo 4:10). ''Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote. Hii ndiyo amri iliyo kuu, tena ni ya kwanza'' (Mathayo 22:37-38). ''nawe mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote'' (Marko 12:30). ''Msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu yeye peke yake'' (Luka 4:8).

Baada ya kufufuka kwake Yesu, Kanisa la Agano Jipya lilifundisha amri ya kwanza:

Paulo alisema, '' Mungu aliyeufanya ulimwengu na vitu vyote vilivyomo…wamtafute Mungu'' (Matendo 17:24, 27). Paulo pia alisema, ''ninavyomwabudu Mungu wa baba zetu, nikiyaamini yote yanayopatana na torati'' (Matendo 24:14). ''Tena pana mapato gani kati ya hekalu la Mungu na sanamu?'' (2 Wakorintho 6:16). ''jinsi mlivyogeukia Mungu mkiaziacha sanamu, ili kumtumikia Mungu aliye hai, wa kweli'' (1 Wathesalonike 1:9). ''Mtu ye yote asiwadanganye kwa njia yo yote; mwana wa uharibifu; yule mpingamizi, ajiinuaye nafsi yake juu ya kila kiitwacho Mungu ama kuabudiwa; hata yeye mwenyewe kuketi katika hekalu la Mungu, akijionyesha nafsi yake kana kwamba yeye ndiye Mungu'' (2 Wathesalonike 2:3-4). ''Msiipende dunia, wala mambo yaliyomo dunia. Mtu akiipenda dunia, kumpenda Baba hakumo ndani yake'' (1 Yohana 2:15); ambayo pia ni njia nyingine ya kusema kwamba usiweke kitu chochote mbele katika ulimwengu kumliko Mungu. ''Mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake, yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu'' (Ufunuo 14:9-10). ''Kisha nikaona viti vya enzi, wakaketi juu yake, nawe wakapewa hukumu; nami nikaona roho zao waliokatwa vichwa kwa ajili ya ushuhuda wa Yesu, na kwa ajili ya neno la Mungu, na hao wasiomsujudia yule mnyama, wala sanamu yake'' (Ufunuo 20:4). ''Bali…wasioamini…na hao waabuduo sanamu…wote, sehemu yao ni katika lile ziwa liwakalo moto na kiberiti. Hii ndiyo mauti ya pili'' (Ufunuo 21:8).

Licha ya kwamba amri ya kwanza siyo ya muhimu sana, tunapata kwamba ndiyo imekiukwa zaidi.

Yesu alipanua uelewa wa amri ya kwanza kwa kusema kwamba kumpenda Mungu ndiyo amri kuu kwa amri zote.

Ni mbaya sana kuasi Mungu kwa kukiuka amri ya kwanza:

22 je! BWANA huzipenda sadaka za kuteketezwa na dhabihu sawasawa na kuitii sauti ya BWANA? Angalia, kutii ni bora kuliko dhabihu, Na kusikia kuliko mafuta ya beberu. 23 Kwani kuasi ni kama dhambi ya uchawi. (1 Samueli 15:22-23)

Mungu anatarajia kwamba watu wake wamtii.

Twapaswa kumpenda Muumba wetu na Baba yetu wa mbinguni. Amri ya kwanza ni ukumbusho ili tufanye hivyo.

Tafuta kwanza ufalme wa Mungu na haki yake (Mathayo 6:33)-weka tumaini lako kwa Mungu (Mithali 3:5-6) na ujaribu kuitunza amri ya kwanza.

# JISOMEE KOZI YA BIBLIA



# Somo la 14b: Je, Wanadamu ni Nani?

**Bob Thiel, Mhariri Mkuu**
Imechapishwa na Kanisa la Mungu *Linaloendelea*

Utangilizi:Kozi hii inatokana kwa kiwango kikubwa na Kozi kwa Mawasiliano iliyohaririwa mwaka wa 1954, iliyoanza chini ya usimamizi ya hayati C. Paul Meredith kupitia Kanisa la Mungu la Redio. Baadhi ya maeneo yake yameboreshwa ili yaendane na karne ya 21 (japo mengi ya maandishi ya awali yamebaki yalivyo).Kadhalika imeongezewa vifungu toka Maandiko Matakatifu, pamoja na taarifa na maswali ambayo hayakuwemo katika kozi ya awali. Maandiko mengi ya Biblia mara nyingi yatoka kwa New King James Version, yanatumika kwa idhini. NKJ pia inatumika. Pia, tafsiri zilizoidhinishwa za Kikatoliki kama vile New Jerusalem Bible (NJB) wakati mwingine inatumika kama vile tafsiri zingine. Anayetafsiri pia hutumia NBT (Neno Biblia Takatifu).

## Mungu Anadhihirisha Jinsi Wanadamu Walivyo!

Yesu Kristo ndiye Neno la Mungu, Msemaji wa Mungu Muumba aliye Mkuu. Kama asingetufunulia maarifa yake, hatungekuwa na uwezo wo wote wa kujua jinsi wanadamu walivyo, maana ya kifo, na yale yatakayotupata mbeleni! Na pasipo kukubali ufunuo wa maarifa hayo, HAUNA msingi wo wote kwa maarifa ama imani yo yote jinsi ulivyo!

Biblia peke yake ndiyo ina rekodi kamili na YENYE HAKIKA ya ushuhuda wa Yesu kuhusu uhai na mauti.

Hili ni neno la Kristo mwenyewe: ''Mimi ni yeye aliye hai, NILIYEKUWA NIMEKUFA''-Kristo baadaye, ametoka kwa wafu, na akawa hai ili ADHIHIRISHE kilichofanyika UPANDE ULE WA MAUTI-'' ni hai milele na milele. Amina. '' Anaendelea kusema, ''Nami ninazo funguo za mauti(kaburi) na kuzimu'' (Ufunuo 1:18).

Kristo ana funguo za kaburi na mauti. Hakuna kitu kinachoweza kufichwa kwake, ama kusitirika chini ya uwezo wake mkuu! Anayo maarifa YOTE; SAYANSI inaweza kufunua SEHEMU kidogo tu ya ukweli ambao Kristo anayajua. Hata hivyo Sayansi inaweza kuchangia kitu. Je, Majaribio ya kisayansi yanasababisha wanasayansi kuamini nini?

SAYANSI INAHUSIKA TU NA VIFAA DUTU-kama vile mata, nguvu, nishati. Mata inaweza kuwa kiumbe hai ama kisicho hai. Sayansi haijui uhai wo wote tofauti na mata, kwa sababu sayansi inahusiana tu na ulimwengu wa vifaa ambavyo vinaweza kuwekwa kwenye mizani na kupimwa-kile kinachoweza kutambulika na hisia tano. Kile ambacho mwanadamu anaweza kukijua KIASILI NI KIFAA KINACHOONEKANA.

HAKUNA MAMLAKA YOYOTE YA KISAYANSI YANAYOAMINI KWAMBA UHAI WA MITI AU WANYAMA NI KITU TOFAUTI AMBACHO KINAWEZA KUWEPO BILA, AU NJE YA MTI AU MNYAMA.

Mchango muhimu ya Sayansi kwenye somo la kujua jinsi wanadamu walivyo ni, SHERIA YA MWANZO WA UHAI. Haya ni maonyesho kwamba viumbe vyote vyenye uhai, au mata vimetokana na vifaa vilivyo hai tayari. Tulizungumzia jambo hili katika Somo la 11 ya Kozi hii. Uhai unaweza kutokea tu kwenye uhai. Wakati uhai umetoweka, mti au mnyama unakuwa kifaa mfu-yaani kifaa kisicho na uhai.

Hakuna kitu kilichoelezwa na Sayansi badala ya kutowezekana kuonekana tena kwa uhai wa mti au mnyama au binadamu-katika ufufuo kupitia kwa nguvu ya asili iliyo ndani ya mata. Hiyo ndiyo baadhi ya sababu inayofanya SAYANSI KUKUBALI KWAMBA hakuna UFUFUO. Sayansi INAWEZA KUTAZAMA KILE AMBACHO KINAONEKANA. Viumbe vyote vilivyo hai vinapatikana na mauti-yaani VINAKUWEPO KWA

MUDA TU. Nyama ni mata na bindamu ni nyama!

Na, je mafundisho ya kutokufa kwa roho? Sayansi inasemaje kuhusu hayo? HAKUNA! SAYANSI HAIJAWAI KUPATA ROHO ISIYOKUFA NDANI YA BINADAMU kwa sababu hakuna njia yo yote SAYANSI inaweza kuchunguza kitu kama hicho. Hakuna ushahidi wo wote katika ulimwengu wote wa uchunguzi wa kisayansi wa kitu chochote kinachoitwa roho isiyokufa ambayo inaacha mwili ukifa na inaondoka na maarifa ambayo imekusanywa katika maisha ya mwanadamu. Kile ambacho sayansi imethibitisha ni kwamba mtu ambaye amekufa kwenye meza ya upasuaji, na akapata ufahamu tena baada ya dakika chache kupitia kwa kuchua musuli wa moyo baada ya kufungua kifua chake kwa haraka, hajui chochote kuhusu wakati alikufa! HAWAJAENDA MAHALI POPOTE! Wanaamka tu kutoka kwenye meza ya upasuaji. Ikiwa dakika nyingi zimepita, utapata kwamba ubongo umezorota kiasi kwamba mtu huyu ananyimwa akili za kufikiria, na hata hazina ya maarifa yake ya awali. Lakini bila shaka hakuna uthibitisho wa roho inayoweza kuwepo bila mwili!

SAYANSI haiwezi kufafanua zaidi ya haya. FILOSOFIA YA MWANADAMU haiwezi kutambua kwa undani, kwa sababu filosofia haiwezi kuthibitisha kisio chochote chake bila vyombo vya sayansi.

BIBLIA PEKEE –ambayo ni Ufunuo wa Yesu Kristo- INAWEZA KUTAMBUA KILE AMBACHO SAYANSI HAIWEZI KUTAMBUA! Yafuatayo basi ni vile Biblia inatambua jinsi MWANADAMU ALIVYO!

1. Je, binadamu ameundwa na nini, kulingana na Yesu Kristo? Yohana 3:6, sehemu ya kwanza. Je, binadamu amezaliwa na mwili wa nyama katika maisha haya? Je, yeye ni NYAMA? Kwa vile binadamu amezaliwa na wazazi wenye mwili wa nyama, basi binadamu HAJAUNDWA kwa ROHO.

MAELEZO: Hapa Yesu anaeleza waziwazi kwamba ikiwa tumezaliwa na mwili, HATUWEZI kuumbwa kwa roho. Binadamu wa kawaida , basi, HAJAUMBWA na ROHO ISIYOKUFA ndani ya mwili unaokufa. Mtu ametengenezwa na mwili unaokufa na wakati mwili huo umekufa, HUYU MTU AMEKUFA-YAANI AMEKUFA KABISA! Sayansi inathibitisha ukweli huo!

2. Je, Yesu Kristo alizaliwa kwa jinsi ya mwili? Warumi 1:3. Kwa hivyo Kristo aliumbwa na mwili, si ndiyo? Linganisha haya na Wakolosai 1:22. Yesu kwa hakika alijua jinsi mwili ulivyo-kwa sababu aliumbwa kwa mwili!

3. Je, Paulo aliumbwa kwa mwili? Warumi 7:18. Je, Paulo ni roho ALIYEVALISHWA katika mwili wa nyama? -ama je, Paulo aliongea kwake yeye mwenyewe kama vile mwili wake ulivyo? Kwa hivyo Paulo alikuwa na mwili unaokufa sio roho isiyokufa?

4. Je, mawazo ya mtu wa kawaida pia ni mawazo ya kimwili? Wakolosai 2:18, sehemu ya mwisho.

## Jinsi Mwanadanu Aliumbwa

Mungu aliumba binadamu wa kwanza. Mungu anaeleza jinsi alivyofanya ili tujijue sisi vile tulivyo. Aliyefanya kazi ya uumbaji ni Yesu Kristo (Wakolosai 1:16). Yafuatayo ndiyo jinsi alivyoumba binadamu:

1. Je, Mungu aliumba binadamu kwa namna gani? Mwanzo 2:7. Kumbuka kwamba ni mtu-SIO TU MWILI-ambaye aliumbwa! Je, inataja kwamba BINADAMU aliumbwa kutoka mavumbini ama kutoka kwa ROHO?

2. Je, binadamu ameumbwa tu na MWILI wa mavumbini-AU BINADAMU aliumbwa na mavumbi? Mwanzo 3:19, sehemu ya mwisho. Ni nani Mungu anaongea naye katika mstari huu-mwili au mwanadamu? Kwa hivyo twapata ni mwanadamu sio mwili tu, ambaye ameumbwa na mavumbi, sivyo?

3. Je, ni nini ingefanyika kwa mwanadamu baadaye? Mwanzo 3:19, sehemu ya kwanza. Ni nani angerudi kwa mavumbi, je ni mwili wa BINADAMU? Je, Mungu anasema ''mwili wako'' ungerudi kwa mavumbi, au ''WEWE''-BINADAMU MWENYE FAHAMU-utarudi mavumbini-gani kati ya hayo ni ukweli?

4. Baada ya Mungu kuumba binadamu asiyekuwa na uhai na kuumba kila kiungo katika mwili wake, Mungu alifanya nini kumfanya huyo binadamu kuwa HAI? Mwanzo 2:7, katikati ya mstari huo. Je, Mungu alipuliza kitu ndani mwa pua ya binadamu? Ni nini hiyo ALIPULIZA NDANI mwa

pua ya binadamu?

MAELEZO: Mungu alipulizia binadamu ''pumzi ya uhai'-HEWA na UPEPO ambazo zilimpa binadamu uhai! Biblia haisemi kwamba binadamu alikuwa na roho isiyokufa kwa sababu Mungu alipuliza roho kama hiyo ndani ya mwanadamu! Ilikuwa pumzi-hiyo pumzi tunayoipumua leo hii-ambayo iliingiza uhai kwa mwanadamu wa kwanza. Mungu alipuliza hewa au upepo ndani ya mapafu kupitia kwa matundu ya pua, na binadamu akaishi!

5. Je, pumzi hiyo iliyopuliziwa binadamu ndiyo ile pumzi ambayo wanyama na ndege na panya wanayo? Mwanzo 7:21-22. Basi chanzo cha UHAI wa wanadamu, wanyama na ndege ni PUMZI ule wa UHAI, sivyo? Kwa vile hakuna roho isiyokufa ambayo inampa uhai wanyama na hata ndege wa angani, basi hakuna roho isiyoweza kufa ambayo inampa wanadamu uhai, je kunayo?

6. Nini inafanyika ikiwa mwili ulio hai umenyang'anywa pumzi ya uhai? Zaburi 104:29, sehemu ya mwisho. Je miili hiyo inakufa? Je, miili yao inarudi mavumbini? Mstari huo huo.

7. Ni nini Zaburi 146:4 inadhihirisha kuhusu uhai wa wanadamu? Nini inarudi mavumbini wakati pumzi imetoka? Ni mwili au ni binadamu? Ni mtu kwa ujumla? Je, fikra za mtu zinaendelea kuwepo katika roho isiyoweza kufa-au fikra ZINAPOTEA? Je, KUPOTEA kunamaanisha kuwepo milele, au KUKOSA kuwepo? (Tazama maana ya kupotea katika kamusi yako).

## Binadamu ni Roho INAYOKUFA

1. Wakati Mungu alipuliza hewa au pumzi katika matundu ya pua, je, Adamu alikuwa nini? Mwanzo 2:7 NKJ, sehemu ya mwisho.

MAELEZO: Neno la awali la Kiebrania ambalo lilitafsiriwa ''roho'' hapa katika KJV , ni ''nephesh. ''Kamusi Rejea ya Young inafafanua neno hili kama ''kiumbe kinachopumua. ''NKJ inatafsiri neno hilo kuwa ''kiumbe. '' Katika Mwanzo 1:21, 24; 2:19; 9:10, 12, 15, 16 na Walawi 11:46 ni neno sawa na ''nephesh'' linalotafsiriwa likiashiria wanyama. Kwa hivyo mwanadamu ni kiumbe.

''Roho, '' nephesh katika Kiebrania, inamaanisha ''uhai'' au ''kiini cha uhai''-kile ambacho kinatufanya tuwe viumbe hai. Neno hilo pia limetumika kwa wanyama katika Biblia-kwa hakika limetumika kwa wanyama kuliko wanadamu katika Agano la Kale (k. v. Mwanzo 1:20, 21, 24).

Kumbuka kwamba neno ''nephesh'' limetafsiriwa kama ''mwili mfu'' au ''mfu'' katika Mambo ya Walawi 19:28; 21:1; 22:4; Hesabu 5:2, 6:11 na 9:6, 7. ROHO BASI NI UHAI WA MNYAMA, AMBAO UKO CHINI YA UOZO NA KIFO, HIYO ROHO INAKUFA.

ROHO IMEUMBWA NA MAVUMBI ya ardhi-ni kifaa siyo kitu cha kiroho. Ni mata. Wakati mwanadamu ANAPUMUA, yeye ni roho ILIYO HAI. Wakati mwanadamu amekoma kupumua, anakufa au anakuwa na roho mfu. Huo ndio ukweli ambao Biblia yako inafunua!

Je, roho inaweza kufa? Ezekiel 18:4 na 20. Ikiwa roho inaishi milele, basi haingekufa, ingekufa kweli? Kwa hivyo roho INAKUFA, sivyo? Ayubu 4:17.

MAELEZO: Kwa vile roho inakufa, kwa hivyo wanadamu WANAKUFA-wako chini ya KIFO.

1. Je, Adamu pia alikuwa chini ya kifo? Mwanzo 2:17, sehemu ya mwisho. Je, ulikuwa ni mwili tu ndio ungekufa au baada ya kifo alikuwa na fahamu?

2. Je, kile kinachowatukia wanadamu pia kinawatukia wanyama? Mhubiri 3:19. Ni nini vile vile kinawatukia wanyama na wanadamu pamoja? Mstari huo. Kwa nini? -kwa sababu wote wana chanzo KISICHODUMU cha uhai, ambacho ni hewa? Je, wanadamu na wanyama wote wanapumua hewa kutoka kwenye chanzo kimoja? Ukija katika maisha ya kawaida, mwanadamu hana uhai kushinda mnyama, si ndiyo?

3. Je, wote wanaenda mahali pamoja wakifa? Mhubiri 3:20. Je, tukio hili lahusu wanadamu WOTE pamoja na wanyama? Wakati mnyama amekufa, hakika amekufa; PIA MWANADAMU AKIFA AMEKUFA pia. Wakati mwanadamu amekufa, bila shaka amekufa kabisa.

4. Ni wapi wanadamu wote na wanyama wanarudia?

Mstari huo wa juu. Je, wote wanarudia mavumbini? Je, huu mstari unasema kwamba mwili peke yake unarudia mavumbi? Je, ni mwili peke yake au ni MTU MZIMA ALIYE NA UFAHAMU ndiye aliyeumbwa na mavumbi, kwa hivyo ni mwanadamu ndiye anayekufa na kurudi mavumbini, sivyo? Mhubiri 3:19-20. Je, fungu hili pia ni sehemu ya Maandiko? Ni sehemu gani ya Maandiko imetiwa msukumo? 2 Timotheo 3:16. Basi fungu hili katika Kitabu cha Mhubiri LIMETIWA MSUKUMO, sivyo?

MAELEZO: Wengine wanashidania kwamba fungu hili katika Mhubiri ni mawazo ya Suleimani tu, lakini huo sio ukweli. Biblia inathibitisha kuwa dhana hiyo ni uongo.

5. Basi Mhubiri 3:21 inafundisha nini?

MAELEZO: Basi kuna tofauti kati ya wanadamu na wanyama. Wanadamu wana ''roho ya mwanadamu'' ndani yao, walakini wanyama, pamoja na sokwe wengine hawana roho kama hiyo. Ukweli kwamba kuna roho ndani ya mwanadamu unafundishwa katika Agano la Kale na Agano Jipya:

> 8 Lakini imo roho ndani ya mwanadamu, Na pumzi ya Mungu huwapa akili. (Ayubu 32:8)
>
> 11 Maana ni nani katika binadamu ayajuaye mambo ya binadamu ila roho iliyo ndani? (1 Wakorintho 2:11)

Mungu aliwapa wanyama silika, lakini siyo aina ya akili aliyowapa wanadamu (Ayubu 39:13-17). ''Roho ya mwanadamu'' haina dhamiri baada ya kifo (Mhubiri 9:5; Zaburi 6:5).

6. Je, mara nyingi wanadamu wanafanana na hayawani ambao WANAPOTEA? Zaburi 49:12

# UHAI wa Binadamu ni Nini?

BINADAMU NI KIUMBE HAI ambaye anapumua na baadaye hufa-yaani NEPHESH, ama roho iliyo hai/ kiumbe hai, ambaye pua yake inatoa hewa.

Wacha basi tuelewe kazi ya pumzi ya hewa ambayo inatoka kwa mapafu yako. Damu inatiririka kupitia kwenye ukuta wa mapafu ikirudi tena kwa moyo, kama vile inasambaza damu kupitia kwa mishipa ya vena na ateri iliyoko mwilini. Pumzi ya hewa baada ya kupitia kwenye mapafu, inatupatia oksijeni. Oksijeni inafyonzwa ndani ya mfumo wa damu na kwa haraka inaungua ili itengeneze nguvu inayotakikana kuhifadhi joto ya mwili na kazi ya viungo vya mwili vya ndani na misuli. UHAI WA MWANADAMU UKO NDANI YA DAMU, na damu inahitaji pumzi ya uhai ili mwili ufanye kazi na kuendelea kuwa hai.

1. JE, NI WAPI UHAI WA VIUMBE VYOTE VILIVYO HAI UNAISHI? Mwanzo 9:4. Je, uhai wa mwanadamu na wanyama wanapatikana ndani ya MFUMO WA DAMU? -ama yeye ni roho iishiyo milele?

2. Je, twapata tena ufafanuzi wa uhai katika Walawi 17:11 na 14?

3. Je, Kumbukumbu la Torati 12:23 pia inasema hivyo?

MAELEZO: Katika mistari hii, neno la Kiebrania NEPHESH limetafsiriwa ''uhai. '' Neno NEPHESH au roho basi linaweza kumaanisha SEHEMU YA NYAMA ya mwanadamu ama MFUMO WA DAMU ya mwanadamu.

4. Je, Kristo alifanya roho yake kuwa dhabihu ya dhambi? Isaya 53:3. Je alifanikishaje jambo hilo? Mstari wa 12.

MAELEZO: Kristo alijitoa nafsi yake kwa ajili ya dhambi zetu (1 Wakorintho 15:3)-alijitoa roho yake au mwili wake usulubiwe na akaruhusu roho yake au nafsi yake kumwagika!

5. Wakati mtu akifa-yaani akikosa uhai-nini inamtukia? Mhubiri 9:5. Je, wafu wanajuaje?

MAELEZO: Kwa sababu wafu hawafahamu chochote, basi mwanadamu hajazaliwa na roho inayoishi milele ambayo itajua vitu vinavyomtukia karibu baada ya mwili wa nyama kufa.

6. Je, wafu wanaweza kumsifu Mungu? Zaburi 115:17. Je, jambo hili linaweza kufanana na yale ambayo wengi wetu wamefundishwa katika makanisa? Je, makanisa wanaamini na kufundisha Biblia?

7. Je, mtu anaweza kuwa na kumbukumbu lo lote la Mungu katika kifo? Zaburi 6:5.

MAELEZO: KIFO ni KINYUME CHA UHAI. Kifo ni KUKOSA UHAI.

# Je, Mwanadamu ni Mnyama tu wa Kawaida?

1. Kwa vile wanadamu na wanyama wote wanadumisha kuwepo kwao na pumzi sawa ya hewa-je, MWANADAMU NI MNYAMA TU wa kawaida? Je, binadamu ameumbwa kwa mfano wa Mungu? Mwanzo 1:26-27. Je, wanadamu wanapaswa kutawala juu ya viumbe vingine vyote? Mstari wa 26.

2. Je, wanyama waliumbwa kwa mfano wa Mungu au aliwaumba kila mmoja kwa jinsi yake? Mwanzo 1:21, 24, 25.

3. Tofauti na ''roho iliyo ndani ya mwanadamu, '' ni nini inatofautisha wanadamu na wanyama-yaani viumbe vingine vya kiwango cha chini ambavyo Mungu aliviumba? Je, mwanadamu angeumbwa kwa mfano na sura ya Mungu? Je, Mungu aliumba binadamu anayekufa-yaani mwanadamu kwa jinsi yake-yaani jinsi ya Mungu? Mwanzo 1:26-27.

MAELEZO: Maneno ya Kiebrania ya Mwanzo 1:26-27 yanaonyesha mpango mkubwa wa Mungu na kusudi la baadaye atakalowafanyia wanadamu! Wakati Mungu alimwumba Adamu kutoka kwa mavumbi, Adamu alifanywa kwa ''mfano''- yaani sura na umbo la Mungu mwenyewe! Mungu hakuifanya aina yo yote ya viumbe alivyoumba kwa mifano yake.

Kumbuka pia kile ambacho Mungu aliwapa wanadamu wakati wa uumbaji! ''Mungu alisema, na tumfanye mtu katika MFANO WETU...''Maneno ya Kiebrania hapa yanaonyesha zaidi ya mfano na umbo la nje ya Mungu-sura yake-NI ZAIDI YA HAYO! Mfano wa Mungu unaonyesha vipengele vya MAWAZO NA TABIA! Hakuna mnyama aliyepewa zawadi ya nguvu ya mawazo! Hii tabia ya kipekee ya mawazo na tabia ndiyo inatofautisha wanadamu na wanyama!

Mwanadamu SIO MNYAMA WA KAWAIDA! Wanyama wana ubongo peke yake-ubongo wa ajabu na ya kutatanisha ambayo ina kiwango cha kumbukumbu na silika-ambayo Mungu aliumba kwa kila aina ya mnyama. LAKINI WANYAMA HAWANA AKILI YENYE NGUVU NA TABIA AMBAZO MUNGU ALIZIUMBA KWA WANADAMU.

Tazama tofauti hiyo kubwa. Wanyama wana ubongo kama vile wanadamu. Ijapokuwa wanyama HAWANA AKILI YA KUTOA HOJA NA KUFIKIRIA!

Wanyama wanafuata mfumo wa mienendo katika kukula kwao, kutengeneza viota, kuhama, kuzaa-wakitumia SILIKA. Hii silika ambayo Mungu aliumba katika ubongo wao imewekwa kama saa ili iwafanye kuitika BILA KUJUA.

Kwa mfano, maelfu ya ndege wanakusanyika kusini wakati majira ya baridi yanakaribia katika kizio cha kaskazini kila mwaka BILA KUJUA, bila kupanga mbeleni mahali watatua. Ijapokuwa kwa kila ishara-kama vile kengele ya saa-wanaacha sehemu yao ya kukula wakati wa kiangazi kule kaskazini na kusafiri maili mengi hadi kusini. Wanasayansi hawaelewi ni kwa nini wanafanya hivyo-wanaweza kuangalia tu shughuli za silika ya mnyama ambaye Mungu aliumba. Kila aina ya ndege-kila aina ambaye Mungu aliumba-ana mifumo ya silika tofauti, wanajenga viota tofauti, wanakula vyakula tofauti, na wanahama kwa njia tofauti na kwa wakati tofauti na kuenda mahali tofauti. Hakuna mnyama ye yote anayepanga vitendo kama hivi, hata hivyo ni itikio ambayo Mungu Mwenyezi aliijenga ndani ya lisika la kila mnyama wakati wa uumbaji.

Lakini BINADAMU ni TOFAUTI! Binadamu anaweza kuona-kutambua na kuelewa-njia nyingi ya kufanya jambo moja. Binadamu anaweza kutoa sababu kwa ukweli na maarifa ambayo ameyakiri, kufikia hitimisho, kufanya uamuzi na kuwa na matendo kulingana na mpango alioufikiri. Wanyama wana uwezo duni sana ya kutoa sababu.

Kila mtu anaweza kujenga nyumba tofauti, kula vyakula tofauti-kuishi kwa njia tofauti sana na wengine. Ikiwa mwanadamu anataka kubadilisha njia fulani ya maisha, basi hiyo inaweza kufanyika! Wanadamu hawako chini ya aina ya silika, ambayo inaongozwa na mkusanyiko wa kanuni za kawaida zilizopangwa mapema, kama vile wanyama.

Wanadamu wanaweza KUCHAGUA-WANADAMU WANA UHURU WA KUCHAGUA! Wanadamu wanaweza kubuni kanuni ya maadili na kuwa na nidhamu ya kibinafsi. Wanadamu wanaweza kuanzisha dhana na kutathmini maarifa ya kisayansi kwa sababu wanadamu wana AKILI iliyofanywa kwa mfano wa Mungu mwenyewe! Wanadamu wanaweza

kubuni, kupanga na kufanya mipango hiyo kufaulu-kwa sababu wanadamu  wana nguvu zingine za ubunifu kama za Mungu mwenyewe! LAKINI NGUVU ZA WANADAMU NI NDOGO KWA WAKATI HUU (Waebrania 2:8).

Sifa za akili na tabia zinafanya wanadamu kuwa uumbaji wa kipekee wa Mungu. Mungu amegawa tabia zake zingine-mfano wa akili yake-kwa mwanadamu-akitarajia wanadamu kupenda na kukuza MFANO KAMILI YA TABIA TAKATIFU YA MUNGU.

Hilo ndilo kusudi la ajabu Mungu anafanya hapa duniani! Mungu aliwapa binadamu uwezo wa kuchagua mema na mabaya-na anawaamuru watu wachague MEMA! Kwa kuzidi kuchagua njia za Mungu-kufanya uamuzi mwema, binadamu atakuwa na tabia sawa na Mungu Mwenyezi!

Hiyo ndiyo binadamu aliumbwa katika uumbaji awe na tabia hiyo. Hiyo ndiyo sababu kuu iliyofanya binadamu kuumbwa tofauti na wanyama, na kupewa-KWA  KIASI-tabia zingine za Mungu!


Mpango wa Mungu ni kuwaumba wanadamu-sasa tu kwa aina ya Mungu katika UDONGO wa kufinyanga-ili washiriki katika tabia tukufu wa Mungu! Mungu anaendelea kujiumba NDANI YA MWANADAMU-na wanadamu wanaobadilisha tabia siku moja wanapandishwa ili wawe AINA ya Mungu!

Ili kuelewa zaidi juu ya kusudi la ajabu la Mungu kwa wanadamu, unapaswa kusoma ''What is the Meaning of Life? '' makala hii inapatikana kwenye tovuti ya COGwriter. com. Kusudi la maisha ya binadamu ndiyo kiini kikuu cha injili ya Yesu. Ndiyo maana watu ambao hawakuelewa ujumbe wake walimstaki kwa KUFUKURU!


---

## Vitabu vya bure vya Kanisa la Mungu *Linaloendelea*


www. ccog.org/books




Christians: AMBASSADORS




Continuing History of the Church of God




Dating: A Key to Success in Marriage




Faith for Those God has Called and Chosen




The Gospel of the Kingdom of God



Is God Calling You?




Is God's Existence Logical?



Prayer: What Does the Bible Teach?

# Ni Injili GANI YESU ALIHUBIRI?




**Na Bob Thiel**

Wakati watu wengi wanajifanya kana kwamba habari njema inahusu nafsi ya Yesu, ukweli ni kwamba wafuasi wa Yesu walifundisha injili ya Ufalme wa Mungu.

Biblia inafundisha kwamba Jamii Timilifu inyoitwa Ufalme wa Mungu itachukua nafasi ya serikali za wanadamu (Danieli 2:44; Ufunuo 11:15; 19:1-12).

Wakati Yesu alianza huduma yake ya umma, alianza na kuhubiri kuhusu Injili ya Ufalme wa Mungu. Yafuatayo ni ripoti ya Marko:

> 14 Hata baada ya Yohana kutiwa gerezani, Yesu akaenda Galilaya, akiihubiri Habari Njema ya Mungu, 15 akisema, Wakati umetimia, na Ufalme wa Mungu umekaribia; tubuni na kuiamini Injili (Marko 1:14-15).

Neno injili, linatoka kwa neno la Ugiriki ambalo limetafsiriwa kama eungelion, na linamaanisha ''ujumbe mzuri'' ama ''habari njema. '' Katika Agano Jipya, neno la Kiingereza la ''Ufalme'' ambalo linahusiana na Ufalme wa Mungu, limetajwa karibia mara 149 katika Biblia ya Kiingereza ya NKJV na mara 151 katika Bblia ya Kiingereza ya Douay Rheims. Linatoka kwa neno la Ugiriki linalotafsiriwa kama basileia ambalo linaonyesha utawala ama milki ya wafalme.

Falme za wanadamu, kama vile Ufalme wa Mungu, una mfalme (Ufunuo 17:14), zinachukua eneo la kijiografia (Ufunuo 11:15), zina sheria (Isaya 2:3-4; 30:9), na zina watu wanaotawaliwa (Luka 13:29).

Hapa ndipo mafundisho ya hadharani kutoka kwa Yesu ambayo Mathayo anarekodi:

> 23 Naye alikuwa akizunguka katika Galilaya yote, akifundisha katika masinagogi yao, na kuihubiri Habari Njema ya ufalme (Mathayo 4:23).

Mathayo pia anarekodi:

> 35 Naye Yesu alikuwa akizunguka katika miji yote na vijiji, akifundisha katika masinagogi yao, na kuihubiri habari njema ya ufalme (Mathayo 9:35).

Agano Jipya linaonyesha kwamba Yesu atatawala milele:

> 33 Ataimiliki nyumba ya Yakobo hata milele, na ufalme wake utakuwa hauna mwisho (Luka 1:33).

Luka anarekodi kwamba  kusudi lililomfanya Yesu kutumwa ni kuhubiri Ufalme wa Mungu. Kumbuka alivyofundisha Yesu:

> 43 Akawaambia, Imenipasa kuihubiri habari njema ya ufalme wa Mungu katika miji mingine pia; maana kwa sababu hiyo nalitumwa (Luka 4:43).

Je, umewahi kusikia injili hii ikihubiriwa? Je, ushagundua kwamba kusudi kuu la Yesu kutumwa ni kuihubiri Injili ya Ufalme wa Mungu?

Luka pia anarekodi kwamba Yesu aliendа na kuihubiri injili ya Ufalme wa Mungu:

> 10 Basi wale mitume waliporudi walimweleza mambo yote waliyoyatenda; akawachukua, akaenda nao faraghani mpaka mji mmoja uitwao Bethsaida. 11 Na makutano walipojua walimfuata; akawakaribisha, akawa akisema nao habari za ufalme wa Mungu (Luka 9:10-11).

Yesu alifundisha kwamba Ufalme wa Mungu unapaswa kuwa kipaumbele kwa wale ambao watamfuata:

> 33 Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake (Mathayo 6:33).

> 31 Bali utafuteni ufalme wa Mungu, na hayo mtaongezewa. 32 Msiogope, enyi kundi dogo; kwa kuwa Baba yenu ameona vema kuwapa ule ufalme (Luka 12:31-32).

Wakristo wanafaa KUTAFUTA KWANZA Ufalme

wa Mungu. Wanafanya hivi kwa kuiweka kama kipaumbele cha juu na kuishi kama Kristo angewahitaji waishi na kutazama kurudi kwake na Ufalme wake. Na bado, wengi wanaokiri Kristo, siyo kwamba hawatafuti kwanza ufalme pekee lakini hawajui hata ufalme huo. Wengi wanaamini kimakosa kwamba kushiriki katika siasa ya ulimwengu ndiyo Mungu anatarajia kutoka kwa Wakristo. Kwa kukosa kuelewa Ufalme wa Mungu, hawaishi sasa vile wanavyotakikana kuishi au hawaelewi kwa nini binadamu wamekuwa na dosari. Kumbuka kwamba ufalme utapewa kundi dogo (Warumi 11:5). Inahitaji uvumilivu ili uwe sehemu ya kundi dogo la ukweli.

## Ufalme wa Mungu Bado Hujaanzishwa hapa Duniani

Yesu alifundisha kwamba wafuasi wake wanapaswa kuomba ili ufalme uje, lakini bado hajaumiliki:

> 9 Baba yetu uliye mbinguni. Jina lako litukuzwe. 10Ufalme wako uje. Mapenzi yako yatimizwe(Mathayo 6:9-10)

Yesu aliwatuma wanafunzi wake wahubiri Ufalme wa Mungu:

> 1 Akawaita wale Thenashara, akawapa uwezo na mamlaka juu ya pepo wote na kuponya maradhi. 2 Akawatuma wautangaze ufalme wa Mungu, na kupoza wagonjwa (Luka 9:1-2).

Yesu alifundisha kwamba kuwepo kwake peke sio ufalme, kwa vile ufalme haukuwa umesimamishwa hapa duniani wakati huo:

> 28 Lakini mimi nikitoa pepo kwa Roho wa Mungu, basi ufalme wa Mungu umekwisha kuwajilia. (Mathayo 12:28)

Ufalme wa ukweli utakuja wakati ujao. Haupo hapa wakati huu kama vile maandiko haya kutoka kwa Marko yanayoonyesha:

> 47 Na jicho lako likikukosesha, ling'oe, ulitupe; ni afadhali kuingia katika ufalme wa Mungu, una chongo, kuliko kuwa na macho mawili, na kutupwa katika jehanamu (Marko 9:47)

> 23 Yesu akatazama kotekote, akawaambia wanafunzi wake, Jinsi itakavyokuwa shida wenye mali kuingia katika ufalme wa Mungu. 24 Wanafunzi wakashangaa kwa maneno yake. Yesu akajibu tena, akawaambia, Watoto jinsi ilivyo shida wenye kutegemea mali kuingia katika ufalme wa Mungu! 25 ni rahisi ngamia kupenya katika tundu ya sindano kuliko tajiri kuingia katika ufalme wa Mungu. (Marko 10:23-25).

> 25 Amin, nawaambia ninyi, Sitakunywa tena kabisa uza wa mzabibu, hata siku ile nitakapokunywa mpya katika ufalme wa Mungu(Marko 14:25).

> 43 akaenda Yusufu, mtu wa Arimathaya, mstahiki, mtu wa baraza ya mashauri, naye mwenyewe anautazamia ufalme wa Mungu, akafanya ujasiri...(Marko 15:43).

Yesu alifundisha kwamba ufalme kwa sasa sio sehemu ya ulimwengu huu uliopo:

> 31 Hapo atakapokuja Mwana wa Adamu katika utukufu wake, na malaika watakatifu wote pamoja naye, ndipo atakapoketi katika kiti cha utukufu; 32 na mataifa yote watakusanyika mbele zake; naye atawabagua kama vile mchungaji abaguavyo kondoo na mbuzi 33 ataweka kondoo mkono wake wa kuume, na mbuzi mkono wake wa kushoto. 34 Kisha mfalme atawaambia wale walioko mkono wake wa kuume, Njoni mliobarikiwa na Baba yangu, urithini ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa ulimwengu (Mathayo 25:31-34).

Kwa vile Ufalme wa Mungu haupo hapa, hatutaona ukamilifu hadi usimamishwe. Kwa sababu wengi hawaelewi Ufalme wa Mungu, wanakosa kuelewa vile serikali ya upendo inafanya kazi.

Ufalme wa Mungu huwezi kuja ''kabla ya ukamilifu wa watu wa Mataifa kufika'' (Warumi 11:25)-na huo bado haujafanyika bado.

Yesu Alisema Ufalme Umefananishwa na Nini?

Yesu alitoa maelezo mengine ya kufananisha Ufalme wa Mungu:

> 26 Akasema, Ufalme wa Mungu, mfano wake ni kama mtu aliyemwaga mbegu juu ya nchi; 27 akawa akilala na kuondoka, usiku na mchana, nayo mbegu ikamea na kukua, asivyojua yeye. 28 Maana nchi huzaa yenyewe; kwanza jani, tena suke, kisha ngano pevu katika suke. 29 Hata matunda yakiiva, mara atapeleka mundu, kwa

kuwa mavuno yamefika (Marko 4:26-29).

> 18 Kisha alisema, Ufalme wa Mungu umefanana na nini? Nami niufananishe na nini? 19 Umefanana na punje ya haradali aliyotwaa mtu akaitupa katika shamba lake, ikamea ikawa mti; ndege wa angani wakakaa katika matawi yake. 20 Akasema mara ya pili, Niufananishe na nini Ufalme wa Mungu? 21 Umefanana na chachu aliyotwaa mwanamke akaisitiri ndani ya pishi tatu za unga, hata ukachacha wote pia (Luka 13:18-19).

Mifano hii inaonyesha kwamba, mwanzoni, Ufalme wa Mungu ni mdogo, lakini utakuwa mkubwa. Luka pia alirekodi:

> 29 nao watakuja watu toka mashariki na magharibi, na toka kaskazini na kusini, nao wataketi chakulani katika ufalme wa Mungu (Luka 13:29).

Kwa hivyo, Ufalme wa Mungu utakuwa na watu kutoka ulimwenguni kote. Hakutakuwa wa Ukoo wa Israeli pekee. Watu watakaa katika ufalme huu.

## Luka 17 na Ufalme

Luka 17:20-21 inatatiza wengine. Lakini kabla hatujafikia haya, kumbuka kwamba watu watakula katika Ufalme wa Mungu:

> 15 ''Heri yule atakayekula mkate katika ufalme wa Mungu'' (Luka 14:15).

Kwa kuwa watu (katika nyakati zijazo) watakula katika ufalme wa Mungu, siyo kitu ambacho kimetengwa katika mioyo yao sasa, licha ya utafsiri mbaya/kukosa kuelewa Luka 17:21 ambacho kinapendekeza kingine.

Tafsiri ya Mofati ya Luka 17:20-21 inafaa isaidie wengine kuelewa:

> 20 Yesu alipoulizwa na Mafarisayo Ufalme wa Mungu utakuja lini, yeye akawajibu, ''Ufalme wa Mungu hauji kwa kuchunguza kwa bidii, 21 wala watu hawatasema, ''Huu hapa, '' au ''Ule kule, '' kwa maana Ufalme wa Mungu umo ndani yenu. (Luka 17:20-21, Mofati; tazama pia tafsiri za ESV)

Kumbuka kwamba Yesu alikuwa akiongea na Mafarisayo ambao hawakuwa wamebadilika, wenye nia ya mwili na wanafiki. Yesu, ''aliwajibu,''- Mafarisayo ndio waliuliza Yesu swali. Walikosa kumtambua.

Je, walikuwa KANISANI? Hamna!

Yesu pia hakuwa akiongea kuhusu kanisa ambalo lingeanzishwa. Na hata hakuwa akiongea juu ya hisia ya mawazo au moyo.

Yesu alikuwa akiongea juu ya UTAWALA wake! Mafarisayo hawakumwuliza kuhusu kanisa. Hawakujua chochote kuhusu Kanisa la Agano Jipya ambalo lingeazishwa hapo baadaye. Hawakumwuliza aina ya mawazo mazuri.

Ikiwa mtu anafikiri kuwa Ufalme wa Mungu ni KANISA-na kwamba Ufalme wa Mungu ulikuwa ndani ya Mafarisayo-Je, KANISA lilikuwa ndani ya Mafarisayo? Hapana!

Hitimisho kama hilo ni hafifu, sivyo? Wakati tafsiri nyingine za Waprotestani zinatafsiri sehemu ya Luka 17:21 kama '' Ufalme wa Mungu umo ndani yenu'' (NKJV/KJV), hata Biblia ya Kikatoliki inayoitwa Biblia ya Yerusalemu Mpya inatafsiri kisahihi kwamba ''ufalme wa Mungu u katikati yenu. ''

Yesu alikuwa katikati ya Mafarisayo. Sasa Mafarisayo wakafikiria wanatarajia kuona Ufalme wa Mungu. Lakini hawakuelewa ufalme huo. Yesu alieleza kwamba ufalme hautakuwa wa kawaida ama wa Wayahudi pekee, kama vile walivyofikiria (ama Kanisa kama vile wengine wanavyodhani sasa). Ufalme wa Mungu hautakuwa tu kama ufalme moja kati ya falme nyingi za wanadamu na falme zinazoonekana ambazo watu wanaweza kuonyesha ama unaoweza kuonekana, na mtu kusema, ''huu ndio ufalme, '' ama ule ndio Ufalme, ni ule pale. ''

Yesu Mwenyewe alizaliwa kuwa MFALME wa huo Ufalme, vile alivyomwambia Pilato waziwazi (Yohana 18:36-37). Ujue kwamba Biblia inatumia neno ''mfalme'' ama ''ufalme'' kwa kubadilishana (k. v. Danieli 7:17-18, 23). MFALME wa Ufalme ujao alikuwa akisimama karibu na Mafarisayo. Lakini hawakumtambua kama mfalme wao (Yohana 19:21). Atakaporudi, ulimwengu utamkataa (Ufunuo 19:19).

Yesu aliendelea mbele katika mistari inayofuata ya Luka 17, kueleza kurudi kwake mara ya pili, wakati Ufalme wa Mungu utatawala DUNIA NZIMA (tukiendelea na tafsiri ya Mofati ili tuwe na uthibiti):

> 22 Kisha Yesu akawaambia wanafunzi wake,

''Wakati utafika ambapo mtatamani kuiona moja ya siku ya Mwana wa Adamu, lakini hamtaiona. 23 Watu watawaambia, ''Yule kule!'' Au, '''Huyu hapa!' Msiwakimbilie. 24 Kwa maana Mwana wa Adamu katika siku yake atakuwa kama umeme wa radi, umulikao katika anga kuanzia mwisho mmoja hadi mwingine. 25 Lakini kwanza itampasa kuteseka katika mambo mengi na kukataliwa na kizazi hiki. (Luka 17:22-25, Mofati)

Yesu alitaja umeme wa radi kama vile alivyotaja katika Mathayo 24:27-31, akieleza kuja kwake mara ya pili KUTAWALA ulimwengu wote. Yesu hasemi kwamba watu wake hawatamwona wakati atakaporudi. Watu hawatamtambua kama MFALME na watajaribu kumpiga vita (Ufunuo 19:19)! Wengine watadhani Yesu anawakilisha Mpinga Kristo. Yesu hakusema kwamba Ufalme wa Mungu ulikuwa ndani mwa Mafarisayo wale-aliwaambia kwamba hawatakuwa katika huo Ufalme kwa sababu ya unafiki wao (Mathayo 23:13-14). Na hata hakusema kwamba Kanisa litakuwa Ufalme.

Ufalme ni kitu ambacho wanadamu siku moja watakuja KUINGIA ndani yake-ni kama vile ufufuo wa wenye haki! Ijapokuwa hata Ibrahimu na wazee wengine wa imani hawamo humo bado ( Waebrania 11:13-40). Wanafunzi walijua kwamba Ufalme wa Mungu haukuwamo ndani yao wakati huo, na ungejitokeza kwa njia ifuatayo kama vile invyoonyeshwa baada ya Luka 17:11:

11 Walipoyasikia hayo, aliongeza kusema mfano, kwa sababu alikuwa karibu na Yerusalemu, na wao walidhani ufalme wa Mungu utaonekana mara (Luka 19:11).

## Ufalme Dhahiri Ulikuwa wa Wakati Ujao

Ni jinsi gani unaweza kusema kuwa Ufalme u karibu? Katika sehemu ya kutatua swali hilo, Yesu aliorodhesha matukio (Luka 21:8-28) na akafundisha:

29 Akawaambia mfano; Utazameni mtini na miti mingine yote. 30 Wakati iishipo kuchipuka, mwaona na kutambua wenyewe ya kwamba majira ya mavuno yamekwisha kuwa karibu. 31 Nanyi kadhalika, **mwonapo mambo hayo yanaanza kutokea, tambueni ya kwamba ufalme wa Mungu u karibu** (Luka 21:29-31).

Yesu likuwa akitaka watu wake wafuate matukio ya kiunabii ili wajue wakati ufalme utakuja. Yesu mahali pengine aliwaambia watu wake kuyatazama matukio ya kiunabii (Luka 21:36; Marko 13:33-37). Licha ya maneno ya Yesu, wengi hawaangalii matukio ya ulimwengu yanayohusiana na unabii.

Katika Luka 22 na 23, Yesu tena alionyeshwa akifundisha kwamba Ufalme wa Mungu ni kitu kitakachotimilika katika wakati ujao:

15 ''Akiwaambia, Nimetamani sana kuila pasaka hii pamoja nanyi kabla ya kuteswa kwangu; 16 kwa maana nawaambia ya kwamba siili tena hata itakapotimizwa katika ufalme wa Mungu. 17 Akapokea kikombe, akashukuru akasema, Twaeni hiki, mgawanye ninyi kwa ninyi; 18 Maana nawaambia ya kwamba tangu sasa sinywi mazao ya mzabibu hata ufalme wa Mungu utakapokuja'' (Luka 22:15-18).

39 Na mmoja wa wale wahalifu waliosulubiwa naye alimkufuru na kusema, ''Ukiwa wewe ni Masihi, ujiokoe na utuokoe pia. '' 40 Na mwenzake akamkemea na kumwambia, ''wewe humwogopi hata Mungu? , nawe u katika hukumu iyo hiyo. 41 Nayo ni haki kwetu sisi, kwa kuwa tunapokea malipo tuliyostahili kwa matendo yetu, bali huyu hakutenda lo lote lisilofaa. 42 Na akamwambia Yeshua, ''Bwana wangu unikumbuke utakapokuja katika Ufalme wako. ''43 Lakini Yeshua alimwambia, ''Amina, nakwambia leo utakuwa pamoja nami Paradiso. '' (Luka 23:39-43, Kiarama katika Kiingereza sahihi).

Ufalme wa Mungu haukuja mara baada ya Yesu kuuawa kama vile Marko na Luka wanavyotuonyesha:

43 akaenda Yusufu, mtu wa Arimathaya, mstahiki, mtu wa baraza ya mashauri, naye mwenye anautazamia ufalme wa Mungu; akafanya ujasiri...(Marko 15:43).

51 naye ni mtu wa Arimathaya, mji mmoja wa Wayahudi, tena anautazamia ufalme wa Mungu (Luka 23:51).

Kumbuka kwamba baada ya ufufuo wa kwanza ndio mtu ataweza kuzaliwa mara ya pili katika Ufalme wa Mungu kama vile Yohana anavyorekodi:

3 Yesu, akajibu akamwambia, Amin, amin nakuambia, Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu. 4 Nikodemo akamwambia, Awezaje mtu kuzaliwa, akiwa mzee? Aweza kuingia tumboni mwa mamaye mara ya pili akazaliwa? 5 Yesu akajibu, Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuingia ufalme wa Mungu (Yohana 3:3-5).

Watu wa Mungu peke yake ndio watauona ufalme wa Mungu ambao utakuwa baada ya miaka elfu.

Sasa elewa zaidi kwamba baada ya kufufuka kwa Yesu, alifundisha tena kuhusu Ufalme wa Mungu:

3 wale alipowadhihirishia nafsi yake, kwa dalili nyingi, baada ya kuteswa kwake, ya kwamba yu hai, akiwatokea muda wa siku arobaini, na kuyanena mambo yaliyohusu ufalme wa Mungu (Matendo 1:3).

**Mahubiri ya kwanza na ya mwisho Yesu alitoa yalihusu Ufalme wa Mungu! Yesu alikuja kama mjumbe kufundisha kuhusu Ufalme.**

Yesu alisababisha Mtume Yohana aandike kuhusu Ufalme wa Mungu wa miaka elfu ambao utakuwa duniani. Tazama ailivyoandika Yohana kutoka kwa Yesu:

4 Kisha nikaona viti vya enzi, wakaketi juu yake, nao wakapewa hukumu; nami nikaona roho zao waliokatwa vichwa kwa ajili ya Neno la Mungu, na hao wasiomsujudia yule mnyama, wala sanamu yake, wala hawakuipokea ile chapa katika vipaji vya nyuso zao, wala katika mikononi yao; nao wakawa hai, wakatawala pamoja na Kristo miaka elfu (Ufunuo 20:4).

Wakristo wa awali walifundisha kwamba Ufalme wa Mungu wa miaka elfu utakuwa duniani na utachukua nafasi ya serikali za ulimwengu kama vile Biblia inavyofundisha (Ufunuo 5:10, 11 :15).

Kwa nini wengi hawajasikia zaidi kuhusu Ufalme wa Mungu ikiwa ni muhimu?

Kwa sababu Yesu aliuita Ufalme kuwa ni siri:

11 Akawaambia, Ninyi mmejaliwa kuijua siri ya ufalme wa Mungu, bali kwa wale walio nje yote hufanywa kwa mifano, (Marko 4:11).

Hata leo Ufalme wa Mungu ni siri kwa wengi.

Kumbuka pia kwamba Yesu alisema kwamba mwisho (wa nyakati) utakuja (mara) BAADA ya injili ya Ufalme wa Mungu kuhubiriwa ulimwenguni pote kama USHUHUDA:

14 Tena habari njema ya Ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote, kuwa ushuhuda kwa mataifa yote; hapo ndipo ule mwisho utakapokuja (Mathayo 24:14).

**Kuihubiri Injili ya Ufalme wa Mungu ni muhimu na kunafaa kufanikishwa katika nyakati hizi za mwisho. Ni ''habari njema'' kwa vile inatoa tumaini kamili kutoka kwa maovu yote ya wanadamu, licha ya wanayoweza kufundisha wanasiasa. Ukizingatia maneno ya Yesu, ni wazi kwamba Kanisa la kweli linafaa kuhubiri habari njema ya Ufalme sasa. Hii ndiyo inafaa iwe kipaumbele cha Kanisa.** Ili ifanywe vizuri, lugha mbalimbali zinapaswa kutumika.

Hii ndiyo Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG) linajitahidi kufanya. Na ndiyo maana kijitabu hiki kimetafsiriwa katika lugha mbalimbali.

Yesu alifundisha kwamba wengi HAWATAKUBALI njia yake:

13 Ingieni kwa kupitia mlango ulio mwembamba; maana mlango ni mpana, na njia ni pana iendayo upotevuni, nao ni wengi waingiao kwa mlango huo. 14 Bali mlango ni mwembamba, na njia imesonga iendayo uzimani, nao waingiao ni wachache. (Mathayo 7:13-14)

Injili ya Ufalme wa Mungu inapeleka watu kwa uzima!

Inavutia kugundua kwamba licha ya wengi wanaokiri Ukristo wanaonekana kutovutiwa na dhana kwamba msisitizo wa Kristo ulikuwa juu ya kuhubiri injili ya Ufalme wa Mungu, wanathiolojia wa kawaida na wanahistoria wamekuwa wakielewa kwamba hiyo ndiyo Biblia inafundisha.

Na bado, Yesu mwenyewe alitarajia wanafunzi wake kufundisha Ufalme wa Mungu (Luka 9:2, 60).

Kwa sababu ufalme unaokuja utakuwa juu ya sheria za Mungu, utaleta amani na ustawi-na kuzitii sheria hizo katika nyakati hizi kunaleta amani ya ukweli (Zaburi 119:165; Waefeso 2:15).

Na habari hizi njema ya ufalme zilijulikana katika maandiko ya Agano Jipya.

# DHIKI KUU na WAKATI wa MWISHO wa MATAIFA

**Na Bob Thiel**

Tunakaribia wakati ambapo Dhiki Kuu itaanza. Itakapoanza haitakuwa wakati mwema kwa watu wa Marekani (Danieli 11? 39) na hata Waingereza wenzao (Yeremia 30? 7).

Pia itakuwa ngumu kwa wengi walioko Mashariki ya Kati na Afrika Kaskazini (Danieli 11? 40-43) na hata wengine pia.

Wengi wamekosa uangalifu mno kiasi cha kwamba hawafikiri Dhiki Kuu itatokea. Lakini hilo litakuwa kosa?

> 9 Inukeni, enyi wanawake wenye raha, sikieni sauti yangu, enyi binti za watu msiokuwa na uangalifu, tegeni masikio yenu msikie matamko yangu. 10 Maana mtataabishwa siku kadha wa kadha zaidi ya mwaka, enyi wanawake mliojikinai, kwa maana mavuno ya mzabibu yatakoma, wakati wa kuvuna vitu vya mashamba hautakuja. 11 Tetemekeni, enyi wanawake wenye raha; taabikeni enyi msiokuwa na uangalifu; jivueni, jivueni nguo zenu kabisa, jivikeni viuno nguo za magunia. 12 Watajipiga vifua kwa ajili ya mashamba mazuri, kwa ajili ya mzabibu uliozaa sana. 13 Juu ya nchi ya watu wangu itamea michongoma na mibigili; naam, juu ya nyumba za furaha katika mji ulio na shangwe; 14 maana jumba la mfalme litaachwa; mji uliokuwa na watu wengi utakuwa hauna mtu; kilima na mnara utakuwa makao ya wanyama, milele, furaha ya punda mwitu, malisho ya makundi ya kondoo (Isaya 32? 9-14).

> 14 Wenye dhambi walio katika Sayuni wanaogopa; tetemeko limewashika wasiomcha Mungu; Ni nani kwetu sisi awezaye kukaa na moto ulao; ni nani kwetu sisi awezaye kukaa na moto uteketezao milele? (Isaya 33? 14)

''Wenye dhambi wa Sayuni'' wanaonekana kuwa ni Wakristo wa Laodikia (Ufunuo 3? 14-19) na/ama ukoo wa Israeli.



Biblia inaonyesha kwamba inapinga ''taifa lenye unafiki'' ambalo Mungu atamtuma mfalme wa Ashuru ulioko Ulaya kumdhibu (Isaya 10? 6). Neno hili la ''unafiki'' pia linapatikana kwa Kiebrania katika Isaya 10? 6 na 33? 14.

Mataifa kama Marekani na Uingereza ni wanafiki.

Tazama kitakachotokea wakati wa ''Dhiki Kuu'' kulingana na Yesu?

> 21 Kwa kuwa wakati huo kutakuwapo dhiki kubwa, ambayo haijatokea namna yake tangu mwanzo wa ulimwengu hata sasa, wala haitakuwapo kamwe. 22 Na kama siku hizo zisingalifupizwa, asingeokoka mtu ye yote; lakini kwa ajili ya wateule zitafupizwa siku hizo. 23 Wakati huo mtu akiwaambia, Tazama, Kristo yupo hapa, au yuko kule msisadiki. 24 Kwa maana watatokea

makristo wa uongo, na manabii wa uongo, nao watatoa ishara kubwa na maajabu; wapate kuwapoteza, kama yamkini, hata walio wateule. 25 Tazama, nimekwisha kuwaonya mbele. 26 Basi wakiwaambia, Yuko jangwani, msitoke; yumo nyumbani, msisadiki. 27 Kwa maana kama vile umeme utokavyo mashariki ukaonekana hata magharibi, hivyo ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu. 28 Kwa kuwa po pote ulipo mzoga, ndipo watakapokusanyika tai (Mathayo 24? 21-28).

Dhiki hii itaanza na muhuri wa tano wa Ufunuo?

9 Na alipoifungua muhuri wa tano, nikaona chini ya madhabahu roho zao waliochinjwa kwa ajili ya neno la Mungu, na kwa ajili ya ushuhuda waliokuwa nao. 10 Wakalia kwa sauti kuu, wakisema, Ee Mola, Mtakatifu Mwenye kweli, hata nini kutokuhukumu, wala kuipatia haki damu yetu kwa hao wakaao juu ya nchi?11 Nao wakapewa kila mmoja nguo ndefu, nyeupe, wakaambiwa wastarehe bado muda mchache, hata itakapotimia hesabu ya wajoli wao na ndugu zao, watakaouawa vile vile kama wao. (Ufunuo 6? 9-11)

Kumbuka kwamba muhuri wa tano imefunguliwa na inahusiana na mateso. Kuna mateso ambayo yametabiriwa kwamba yatatokea kabla ya Dhiki Kuu kuanza kulingana na Danieli 7? 25a, 11? 28-35; Ufunuo 12? 13, na hata wakati wa Dhiki Kuu kulingana na Danieli 7? 25a, Ufunuo 12? 17; 14? 1-13.

Tazama yafuatayo kutoka kwenye Kitabu cha Yeremia?

5 Watesi wake wamekuwa kichwa, Adui zake hufanikiwa; Kwa kuwa BWANA amemtesa Kwa sababu ya wingi wa makosa yake; Watoto wake wadogo wamechukuliwa mateka mbele yake huyo mtesi. (Maombolezo 1? 5)

17 Sayuni huinyosha mikono yake; Hakuna hata mmoja wa kumfariji; BWANA ametoa amri juu ya Yakobo, Kwamba wamzungukao wawe watesi wake; Yerusalemu amekuwa kati yao Kama kitu kichafu (Maombolezo 1? 17).

2 Bila huruma Bwana ameyameza makao yote ya Yakobo; katika ghadhabu yake amebomoa ngome za Binti Yuda. Ameungusha ufalme wake na wakuu wake chini ya aibu. 3 Katika hasira kali amevunja kila pembe ya Israeli. Ameundoa mkono wake wa kuume alipokaribia adui. Amemteketeza Yakobo kama moto uwakao ule uteketezao kila kitu kinachouzunguka. 4 Ameupinda upinde wake kama adui, mkono wake wa kuume uko tayari. Kama vile adui amewachinja wote waliokuwa wanapendeza jicho amemwaga ghadhabu yake kama moto juu ya hema la Binti Sayuni. (Maombolezo 2? 2-4, NBT)

11 Macho yangu yamedhoofika kwa kulia, nina maumivu makali ndani, moyo wangu umemiminwa ardhini kwa sababu watu wangu wameangamizwa, kwa sababu watoto na wanyonyao wanazimia kwenye barabara za mji. 12 Wanawaambia mama zao, ‘’Wapi mkate na divai?’’ Wazimiapo kama watu waliojeruhiwa katika barabara za mji, maisha yao yadhoofikavyo mikononi mwa mama zao. (Maombolezo 2? 11-12, NBT)

19 Inuka, lia usiku, zamu za usiku zianzapo; mimina moyo wako kama maji mbele za Bwana. Mwinulie yeye mikono yako kwa ajili ya maisha ya watoto wako, ambao wanazimia kwa njaa kwenye kila mwanzo wa barabara. (Maombolezo 2? 19, NBT)

21 ‘’Vijana na wazee hujilaza pamoja katika mavumbi ya barabarani, wavulana wangu na wasichana wameanguka kwa upanga. Umewauwa katika siku ya hasira yako, umewachinja bila huruma. (Maombolezo 2? 21, NBT)

8 Lakini sasa ni weusi kuliko masizi; hawatambulikani barabarani. Ngozi yao imeshikamana juu ya mifupa yao, imekuwa mikavu kama fimbo. 9 Wale waliuoawa kwa upanga ni bora kuliko wale waliokufa kwa njaa, walitokomea kwa ajili ya kukosa chakula kutoka shambani. 10 Kwa mikono yao wenyewe wanawake wenye huruma walipika watoto wao wenyewe, ambao walikuwa chakula chao wakati watu wangu walipoangamizwa. 11 BWANA ametoa nafasi kamilifu ya ghadhabu yake; ameimwaga hasira yake kali. Amewasha moto katika Sayuni ambao umeteketeza misingi

yake. (Maombolezo 4? 8-11 NBT)

> 15 Furaha imeondoka katika mioyo yetu, kucheza kwetu kumegeuka maombolezo. 16 Taji imeanguka kutoka kichwani petu. Ole wetu, kwa maana tumetenda Dhambi!17 Kwa sababu ya hiyo mioyo yetu inazimia, kwa sababu ya mambo haya macho yetu yamefifia, (Maombolezo 5? 15-17 NBT)

Kwa vile Yesu alisema kwamba hii ndiyo itakuwa dhiki kuu kuliko yote, itakuwa hatari kama vile Yeremia alivyotiwa msukumo kuandika.

Hata hivyo wengi katika Kanisa la Mungu wamepitia mateso ya kiuchumi na kijamii katika kutembea kwao na Kristo, mateso ya hatari, ukianza na mabakio ya Wakristo wa Filadelfia wanavyotarajiwa (Danieli 7? 25a, 11? 28-35), baadaye itafuatwa na dhuluma ya Wakristo wote baada ya Dhiki Kuu (Mathayo 24? 21) wakati utakapoanza.

Je, kila kitu kimekosa matumaini?

La Hasha!

Yeremia pia aliandika?

> 25 BWANA ni mwema kwa hao wamngojeao, Kwa hiyo nafsi imtafutayo. 26 Ni vema mtu autarajie wokovu wa BWANA Na kumngonjea kwa utulivu. (Maombolezo 3? 25-26)

Hata kama nchi yako haitatubu (iwe ni Uingereza ama ingine), wewe mwenyewe unaweza kutubu.

Wakristo wengine, lakini sio wengi watalindwa (Ufunuo 12? 14-17; Ufunuo 3)-ni Wakristo Wanafiladelfia ndio wameahidiwa ulinzi (Ufunuo 3? 7-13).

Wakati wengi wanapenda kuangazia kwamba Wanafiladelfia wataenda mahali pa ulinzi, inapaswa tujue kwamba kutakuwako na mateso kabla hawajatoroka na kabla ya Dhiki Kuu ambayo Wakristo watavumiliana nayo.

Wakati huu pia utakuwa wakati wa ishara za mashetani na miujiza ya uwongo ( 2 Wathesalonike 2? 7-12; Ufunuo 16? 12-16; 13? 13-15; 18? 23; 19? 20).

Tazama maelezo mengine ya Biblia ya matukio yatakayofanyika wakati wa mwisho kwa ukoo wa Israeli?

> 47 kwa kuwa hukumtumikia BWANA, Mungu wako, kwa furaha na moyo wa kushukuru, kwa ajili ya ule wingi wa vitu vyote; 48 kwa hiyo utawatumikia adui zako atakaowaleta BWANA juu yako, kwa njaa, na kwa kiu, na kwa uchi, na kwa uhitaji wa vitu vyote; naye atakuvika kongwa la chuma shingoni mwako, hata atakapokwisha kufa kuangamiza. 49 BWANA atakuletea taifa juu yako kutoka mbali, kutoka ncha ya dunia, kama arukavyo tai; taifa usiloufahamu ulimi wake; 50 taifa lenye uso mkali, ambalo haliangalii uso wa mzee, wala halipendelei kijana; 51 naye atakula uzao wa ng'ombe wako wa mifugo, na uzao wa nchi yako mpaka utakapokwisha kuangamizwa; wala hatakuachia nafaka, wala divai, wala mafuta, , wala maongeo ya ng'ombe wako, wala wanakondoo wako, hata atakapokwisha kukuangamizwa. (Kumbukumbu la Torati 28? 47-51).

> 16 Tena akaniambia, Mwanadamu, tazama, nitalivunja tegemeo la chakula katika Yerusalemu; nao watakula mkate kwa kuupima, na kwa kuutunza sana, nao watakunywa maji kwa kuyapima, na kwa kushangaa; 17 wapate kupungukiwa na mkate na maji, na kuustajabiana, na kukonda kwa sababu ya uovu wao. (Ezekieli 4? 16-17).

1 Nawe mwanadamu, ujipatie upanga mkali, kama wembe wa kinyozi ujipatie, ukaupatishe juu ya kichwa chako na ndevu zako; kasha ujipatie mizani ya kupimia, ukajigawanye nywele hizo. 2 Theluthi ya hizo utaiteketeza katikati ya mji, siku ya mazingiwa zitakapotimia, nawe utatwaa theluthi, na kuipiga kwa upanga pande zote; nawe utatawanya theluthi ichukuliwe na upepo, nami nitafuta upanga nyuma yake. 3 Nawe twaa nywele chache katika hizo, na kuzifunga katika upindo za mavazi yako. 4 Nawe utatwaa tena baadhi ya hizo, na kuzitupa katikati ya moto, na kuziteketeza katika moto huo; kutoka nywele hizo moto utakuja na kuingia katika nyumba yote ya Israeli. 5 Bwana MUNGU asema hivi; Huu ndio Yerusalemu; nimeuweka kati ya mataifa, na nchi zauzunguka pande yote. 6 Nao umeasi hukumu zangu, kwa kutenda mabaya kuliko mataifa hayo, nao umeasi sheria zangu kuliko nchi hizo ziuzungukazo; maana wamezikataa hukumu zangu, wala hawakuenda katika sheria zangu. 7 Basi, kwa hivyo BWANA Mungu asema hivi; kwa ninyi mmefanya ghasia kuliko mataifa wawazungukao

ninyi, wala hamkuenda katika sheria zangu, wala hamkuzishika hukumu zangu, wala hamkutenda kama kawaida za mataifa wawazungukao; 8 basi BWANA Mungu asema hivi, Angalia, mimi, naam, mimi, ni juu yako, nami nitafanya hukumu kati yako machoni pa mataifa. 9 **Nami nitakutenda nisiyoyatenda zamani, wala sitafanya tena mambo kama hayo,** kwa sababu ya machukizo yako yote. 10 Kwa sababu hiyo baba ya watu watawala wana wao kati yako, nao wana watawala baba zao; nami nitafanya hukumu ndani yako, na hao wote waliosalia kwako nitawatawanya kwa pepo zote. 11 Kwa sababu hiyo, kama mimi niishivyo, asema Bwana MUNGU, hakika kwa kuwa umepatia unajisi patakatifu pangu, kwa matendo yako yote niyachukiayo, na kwa machukizo yako yote, kwa sababu hiyo mimi nami nitakupunguza; wala jicho langu halitaachilia, wala sitaona huruma. 12 Theluthi yenu mtakufa kwa tauni, na kwa njaa watakomeshwa ndani yako; na theluthi yenu wataanguka kwa upanga pande zako zote; na theluthi yenu nitawatawanya kwa pepo zote, kisha nitafuta upanga nyuma yao. (Ezekiel 5? 1-12)

Sehemu yenye **herufi nzito** inaambatana na maelezo ya Yesu katika Mathayo 24? 21 na Marko 13? 19, kwa hivyo yaliyo juu hapa yanahusu Dhiki Kuu.

Hata hivyo, licha ya wanavyofikiri wengine, Dhiki Kuu itaathiri sana ukoo wa Yakobo/Israeli?

> 6 Ulizeni sasa, mkaone kwamba mwanamume aona utungu wa uzazi; mbona basi, nikaona kila mtu anaweka mikono yake viunoni, kama mwanamke aliye na utungu, na nyuso zote zimegeuka rangi. 7 Ole! Maana siku ile ni kuu, hata hapana inayofanana nayo, maana ni wakati wa taabu wa Yakobo; lakini ataokolewa nayo. (Yeremia 30? 6-7)

> 25…mataifa wasiokujua…wamemla Yakobo, naam wamemla kabisa na kumwangamiza, na kuyafanya makao yake kuwa ukiwa. (Yeremia 10? 25)

Basi, twaona kwamba Mataifa watamla Yakobo/ Israeli. Ukoo ambao ni watu wapatikanao Marekani,

Uingereza, Kanada, Australia, na Nyuzilandi.

# Uharibifu Mkuu?

Wengine wataiita mwanzo wa Dhiki Kuu kuwa ni Vita vya tatu vya Ulimwengu.

Wengine wanashangaa kwa nini Marekani, nikitaja taifa moja, litaharibiwa. Bila shaka, kwa sababu ya siasa, Marekani wameimarisha ajenda ya mashoga ulimwenguni (hata hivyo ajenda hiyo imepungua kidogo wakati wa utawala wa Trump). Nyingine ni kwamba kwa sababu ya shida za kiuchumi, Marekani imekuwa nchi yenye deni kubwa kuliko yote. Pia kwa sababu ya dhambi, uchoyo na kutojali, Marekani wamekuwa wakitoa mimba na kutengezeza vyakula vya kijenetiki. Vyakula hivi vinafanana na vyaweza kukabiliwa na kuondolewa kabisa na viumbe vinavyosababisha magonjwa. Nimewahi kutuhumu kwamba wakati utafika ambapo aina ya tauni itapiga mazao hayo ya kijenetiki kama ngano na kusababisha uharibifu mkubwa kwenye ardhi. Hayo yatosha kiasi cha kutia hamasa maadui wake kuwashambulia Uingereza na/ama Marekani kuanza Dhiki Kuu.

Mataifa watasaliti Marekani, ambalo lilikuwa ''mkuu miongoni mwa mataifa. ''

> 1 Jinsi mji huu ukaavyo ukiwa, Huo uliokuwa umejaa watu! Jinsi alivyokuwa mkuu kati ya mataifa! Binti mfalme kati ya majimbo, Jinsi alivyoshikwa shokoa! 2 Hulia sana wakati wa usiku, Na machozi yake yapo mashavuni; Miongoni mwa wote waliompenda Hakuna hata mmoja amfarijiye; Rafiki zake wote wamemtenda hila, Wamekuwa adui zake. (Maombolezo 1? 1-2)

> 4 Ni lazima kununua maji tunayokunywa, kuni zetu zinaweza kupatikana tu kwa kununua. 5 Wale ambao wanatufuatilia wapo kwenye visigino vyetu, tumechoka na hakuna pumziko. 6 Tumejitolea kwa Misri na Ashuru tupate chakula cha kutosha. 7 Baba zetu walitenda dhambi na hawapo tena, na sisi tutachukua adhabu yao. 8 Watumwa wanatutawala na hakuna ye yote wa kutuweka huru kutoka katika mikono yao. (Maombolezo 5? 4-8, NBT)

Kumbuka kwamba ''marafiki'' watamsaliti na kwamba Ashuru, ambaye Mungu atatumia kuadhibu ukoo wa Israeli kama vile Marekani n. k. (makabila

mchanganyiko wa Marekani wanaitwa 'Samaria' katika Isaya 10? 5-12); pia wamehusishwa. Ashuru wa kisasa wanajulikana kuwa marafiki/washirika wa Marekani, Kanada, Uingereza n. k.

Uharibifu utalijia kwa ghafula taifa ambalo lina deni kubwa (Marekani ndilo wamekuwa taifa lenye deni kubwa kuliko wengine-na deni yake inatarajiwa kuongezeka)?

> 8...mwenye kuteka wakati wa adhuhuri ; nimeleta hamu na maogofyo yampate ghafula. (Yeremia 15? 8)

> 6 Je! Hawa wote hawatapiga mfano juu yake, na mithali ya kusimanga juu yake, wakisema, Ole wewe aongezaye kisicho mali yake!Hata lini?Na ole wake yeye ajitwikaye mzigo wa rehani! 7 Je! Hawatainuka ghafula wao watakaokuuma, hawataamka wao watakaokusumbua, nawe utakuwa mateka kwao? 8 Kwa sababu umeteka nyara mataifa mengi, mabaki yote ya makabila watakuteka wewe; kwa sababu ya damu ya watu, na kwa sababu ya udhalimu iliotendwa nchi hii, na mji huu, na watu wote wanaokaa ndani yake. (Habakuki 2? 6-8)

Hayati Mchungaji wa Kanisa la Mungu Ulimwenguni Kote (WCG), Herbert W. Armstrong, aliandika yafuatayo katika 1979?

> Ni chukizo gani hili? Hili linaloonyeshwa katika Danieli 11? 31 na Mathayo 24? 15...Huu utakuwa wakati ambapo Ulaya ILIO NA UMOJA itatokea-uamsho wa enzi za kati ya''Utawala wa Rumi Mtakatifu. ''Tutaonywa na kuchukuliwa hadi mahali pa hifadhi na ulinzi ili tuokolowe na Dhiki Kuu. **Baada ya miaka arobaini ''wanajeshi wa mnyama'' watazingira Yerusalemu. Baada ya siku thelathini, Dhiki Kuu itaanza na mashambulizi ya nyuklia kwenye London na Uingereza-na pengine siku hiyo ama mara hiyo, kutakuwepo na mashambulizi ya miji ya Marekani na Kanada.** DHIKI KUU, itatufanya tugundue kwamba huo ndio wakati wa ''Taabu ya Yakobo, '' iliyonenwa katika Yeremia 30? 7. Na jina la Yakobo lilichuliwa na wana wa Yusufu, yaani Efraimu na Manase (Mwanzo 48? 16). Wakati huo theluthi ya watu katika mataifa yetu watakufa, ama watakuwa wamekufa kwa njaa na majanga la magonjwa; theluthi moja ya wengine watakuwa wamekufa kwa vita-na miji yetu itaharibiwa(Ezekieli 6? 6), na theluthi moja ya watu watabebwa na kupelekwa kwa nchi ya maadui wetu kama watumwa (Ezekieli 5? 12). (Armsrong HW. The Time Are In, Now. Pastor General's Report-Vol 1, No. 15, November 20, 1979, Page 2).

Biblia inasema?

> 33 Nany nitawatapanya-tapanya katika mataifa, nami nitaufuta upanga nyuma yenu; na nchi yenu itakuwa na ukiwa, na miji yenu maganjo(Walawi 26? 33).

Nyuklia na zana zingine za vita ama uharibifu wa namna hiyo ni sehemu ya laana ambayo imetajwa katika Biblia?

> 23 ya kuwa nchi yake nzima ni kibiriti, na chumvi, na kuteketea(Kumbukumbu 29? 23).

> 19 Kwa sababu ya hasira ya BWANA wa majeshi nchi hii inateketea kabisa; watu hawa ni kama kuni zitiwazo motoni; hapana mtu amhurumiaye ndugu yake. 20 Hupokonya upande wa mkono wa kuume, nao huona njaa! Hula upande wa mkono wa kushoto, wala hawashibi! Watakula kila mtu nyama ya mkono wake mwenyewe. 21 Manase anamla Efraimu, naye Efraimu anamla Manase; nao wawili pamoja watakuwa juu ya Yuda (Isaya 9? 19-21).

> 6 Kila mahali mkaapo miji itaharibika (Ezekieli 6? 6).

Kutakuwa na uwezekano kwamba Waprotestani wengi ambao wataishi wakati wa dhiki (hata kama waliamini mtazamo wa dhiki kabla ya kurudi kwake Kristo) watakuwa sehemu ya umati wa watu watakaobadilika wakati wa dhiki (Ufunuo 7? 9) kupitia kwa ujumbe wa Kanisa la Mungu Linaloendelea ambao wakati huo utaletwa kwa ulimwengu na ''mashahidi wawili'' (wengi wa Ugiriki-Rumi na madhehebu ambao hawaamini Biblia pia watabadilika; Ufunuo 7? 9-10).

Twajuaje kwamba mataifa ya Kizungu kwa ujumla, na hasa Marekani, na sio nchi ya Yudea ndiyo lengo la awali ya dhiki kuu? Sababu moja ni Danieli 11? 39?

> 39 Naye ataziteka nyara ngome zenye nguvu kwa msaada wa mungu mgeni; na yeye atakayemkubali atamwongeza kwa utukufu; naye atawapa kumiliki wengi naye ataigawa nchi kwa rushwa. (Danieli 11? 39)

Huyo ambaye ametajwa hapo juu ni Mfalme wa mwisho wa Kaskazini, Mnyama wa Ufunuo 13. Katika karne ya 21, ngome zenye nguvu ni za Marekani, na kwa kiwango kingine wazungu walio washirika wake. Ngome zenye nguvu haziwezi kuwa China ama Urusi kwa sababu hawatahusika hadi mstari wa 44 wa Danieli 11. Siyo hata nchi za Warabu kwa sababu wao hawataingiliwa hadi ifike mstari wa 40-43. Taifa la sasa la Israeli , hakika halina ngome zenye nguvu. Na pia kugawanya nchi za wazungu italeta faida , kuliko nchi ya Yudea. Kwa hivyo, jambo hili linaashiria mataifa ya wazungu ambao wanahifadhi watu wengi katika kanisa la kweli.

## Wakati wa Mwisho wa watu wa Mataifa

Wakati wa mwisho wa watu wa Mataifa unaambatana na wakati wa Dhiki Kuu na wakati wa taabu ya Yakobo.

Ili kwamba wakati wa watu wa Mataifa ufike, Mataifa watahitaji kuungana pamoja dhidi ya Marekani na washirika wa ukoo wa Wazungu. BRICS (Brazil, Urusi, India, China, South Afrika), EAEU (Muungano wa Kiuchumi wa Ulaya), SCO (Shirika la Muungano wa Shangai), EU(Umoja wa Ulaya), na Njia Hariri (Mpango wa China wa kuunganisha Asia kupitia kwa barabara na njia za maji) mipango yote imekusudiwa kufanya yote na yote itafungamana na unabii wa kibiblia unaoeleweka vizuri. Kundi la mataifa kutoka Afrika Kaskazini na Mashariki ya Kati, ambayo Rais wa Marekani Donald Trump atahimiza, pia watahusishwa (Danieli 11? 27, 40? 43).

Hata hivyo, watu wengi walioko Marekani, Kanada, Uingereza, Australia na Nyuzilandi hawaelewi kinachofanyika kwa eneo la ulimwengu na hata jinsi watakavyoathirika.

Wacha tuangalie unabii ufuatao kutoka kwa Agano la Kale na Jipya unaohusiana na Mataifa?

> 23 Ufue mnyororo; kwa maana nchi hii imejaa hukumu za damu, nao mji umejaa udhalimu. 24 Kwa sababu hiyo nitawaleta watu wa mataifa walio wabaya kabisa, nao watazimiliki nyumba zao; tena nitakikomesha kiburi chao wenye nguvu; na mahali pao patakatifu patatiwa unajisi. 25 Uharibifu unakuja; nao watatafuta amani, lakini haitapatikana. (Ezekieli 7? 23-25)

> 23 Ole wao wenye mimba na wanaonyonyesha katika siku hizo! Kwa kuwa kutakuwa na shida nyingi katika nchi, na hasira juu ya taifa hili. 24 Wataanguka kwa ukali wa upanga, nao watatekwa nyara na kuchukuliwa katika mataifa yote; na Yerusalemu utakanyagwa na Mataifa, hata majira ya Mataifa yatakapotimia. (Luka 21? 23-24)

> 2 Na behewa iliyo nje ya hekalu uiache nje wala usiipime, kwa maana Mataifa wamepewa hiyo, nao wataukanyaga mji mtakatifu miezi arobaini na miwili. (Ufunuo 11? 2)

Kumbuka kwamba Yeremia, Ezekieli na Yesu (ambaye maneno yake yamerekodiwa katika Luka) na Yohana (ambaye aliandika Ufunuo) walikuwa wakiongea kuhusu wakati mmoja. Pia kumbuka kwamba ''ni wakati wa taabu ya Yakobo'' na kwamba ''Watu wa Mataifa wanatawala'' inamaanisha kwamba ukoo wa Israeli ama wale walio na jina la Yakobo (Mwanzo 48? 14-16) watakanyagwa. Mmoja kati ya watu ambao Mungu anasema atawatumia kuwadhibu ukoo wa Israeli ni Ashuru (Isaya 10? 5-11), ambao ni watu wa Mataifa-wataongoza wakati wa watu wa Mataifa. Huu utakuwa wakati wa hatari.

Yafuatayo ni yale yaliofundishwa na Kanisa la Mungu la Redio kuhusu wakati huo?

> Katika unabii wa Yesu wa Mathayo 24, alikuwa akijibu swali kuhusu WAKATI wa mwisho wa ulimwengu, na kurudi kwake mara ya pili ya Kristo kutawala ulimwengu.

### *NANI ataleta Dhiki?*

> Baadaye, ni NANI ataleta shida hii? NANI atatumbukiza ulimwengu kwenye dhiki hii? Twapaswa kujua ni nani na ni wakati gani?Basi mtambue ni nani! Nabii Yeremia anaongea kuhusu wakati huu wa shida kubwa ''Kwa maana, tazama, siku zinakuja, asema BWANA, nitakapowarejeza watu wangu wa Israeli na

Yuda waliofungwa, asema BWANA; nami nitawarudisha hata nchi niliyowapa baba zao, nao wataimiliki. ’’ (Yeremia 30? 3)...

Endelea na Unabii wa Yeremia? ‘’Maana BWANA asema hivi, Tumesikia sauti ya tetemeko, na ya hofu, wala si ya amani-NI WAKATI WA VITA!... Ole! Maana siku ile ni KUU, hata hapana inayofanana nayo, -Kumbuka kwamba ni wakati wa taabu KUU maana ni wakati wa taabu yake Yakobo. Ukumbuke kwamba si wakati wa taabu ya NANI? Ni wakati wa TAABU YA YAKOBO!. .

Nani aitwaye Yakobo?. . .

Nani Anaitwa Yakobo leo hii?. . .

Mmoja kati ya wana kumi na wawili wa Yakobo, yaani Yusufu, alipewa ‘’sehemu mbili’’ na akawa kabila mbili-Efraimu na Manase-ambao ni wana wawili wa Yusufu. Na hao ndiyo kabila waliopewa haki ya mzaliwa wa kwanza. .

Na ni hawa kabila mbili ndio walipewa JINA Israeli? ‘jina langu na litajwe juu yao’ alisema mzee huyo Israeli (Mwanzo 48? 16), wakati alikuwa akiwapa ahadi ya haki ya mzaliwa wa kwanza mara kabla ya kifo chake. Na kwa hivyo , JINA Yakobo au Israeli, mara nyingi linamaanisha mataifa mawili ambao walitoka kwa Efraimu na Manase. Mataifa haya ni Uingereza na Marekani. NIRA hiyo iliyotabiriwa ya uvamizi, kushindwa kwa vita na utumwa itaangukia Uingereza na Marekani! (Armstrong HW. BRITAIN’S DOOM Prophesied for Common Market Seeking Membership! Plain Truth, July 1962)

## *Mafundisho ya Kawaida ya Urongo*

Ni wazo la kawaida kwamba wakati wa watu wa Mataifa ni wakati wa Baraka ya mataifa. Watu wanasema kwamba kwa vile Mungu aliondoa Baraka ya Israeli na Yuda kuwa kuu na mataifa yanayotawala na kwa vile watu wa Mataifa wamekuwa wakitawala kwa karne nyingi, basi utawala wa bindamu ni Baraka ambayo imetawazwa juu ya watu wa Mataifa.

Kauli hii ni mbali sana na ukweli!. . .

## *Wakati wa Adhabu ya Israeli ni Msingi wa Kuelewa*

Israeli waliahidiwa baraka kubwa ya kitaifa, pamoja na ukuu wa kitaifa ikiwa wangemtii Mungu. Lakini Mungu pia alisema kwamba ikiwa watakataa kwa ukaidi kumtii Mungu, ikiwa watakataa kuzifuata amri zake na kumwacha awatawale maisha yao, basi atawadhibu kwa muda ambao unaitwa mara saba (Walawi 26).

Biblia yenyewe inatufafanulia muda huu unaoitwa mara saba. Ukifungua Ufunuo mlango wake wa kumi na mbili, na ulinganishe mstari wa 6 na 14 utaona kwamba neno wakati katika unabii linamaanisha mwaka, kwa hivyo mara saba itakuwa miaka saba au siku 2520.
Basi wacha tuangalie njia nyingine ya kuelewa unabii huu. Hesabu 14? 34, Mungu alisema Israeli watayabeba maovu yao jangwani baada ya siku ambazo walitafuta nchi ya Kanani, siku arobaini, kila siku kwa mwaka.

Mara saba au siku 2520 ya kinabii basi itakuwa miaka 2520 ya kawaida! Muda huu wa mara saba au miaka 2520 ya adhabu ulimjia Israeli kwa sababu walienda kwenye njia zao wenyewe na hawakuzitii sheria za Mungu. Israeli walipelekwa mateka katika mwaka wa 721 K. K na hawakuwa watu wakuu tena hadi wakati wao wa adhabu ulipofika mnamo mwaka wa 1800 B. K. Kwa wakati huo, uzao wa Nyumba ya Israeli-Marekani na Uingereza na watu wote wakidemokrasia wa ulimwengu-walianza kuinuka kwa mali na nguvu ile ulimwengu haujawahi kufurahia kwa sababu ya ahadi Mungu aliifanya na Ibrahimu.

Pia, Palestina, baada ya adhabu dhidi ya Nyumba ya Yuda, ambayo ilianza mnamo 604 K. K. , walirudishwa kutoka kwa Waturuki ambao ni Mataifa mwaka wa 1917-miaka 2520 baadaye, wakati nchi ya Palestina ilikuja kuwa chini ya utawala wa Uingereza Mkuu na baadaye Wayahudi. Mara saba ya adhabu ya Israeli ulikuwa muda wa ufukara na mateso, wa utumwa na vita kwa sababu hawangewashilisha mapenzi yao kwa Mungu, kwa sababu hawakuruhusu Mungu kutawala maishani mwao kwa sheria zake timilifu, ambazo zingewaletea amani na ustawi na mamlaka.

### *Unabii wa Awali Unaopatikana Katika Kitabu cha Danieli*

Basi kwa vile tunaelewa mara saba ya adhabu kwa Israeli, wacha basi tuelewe maana ya wakati wa watu wa Mataifa.

Unabii wa awali ambao Yesu alionyesha unapatikana katika Mlango wa nne wa Danieli. Yesu alielewa kwamba njozi hii ya kiunabii ya mti mkubwa ilikuwa inaonyesha nyakati za watu wa Mataifa na pia adhabu ya kawaida ya Nebukadreza.

Tazama Danieli 4? 17. Njozi hii ya ajabu haikuwa tu ya kufundisha Nebukadreza kwamba Mungu atatawala, lakini pia ''kusudi watakatifu wapate kujua ya kuwa Aliye juu anatawala katika ufalme wa wanadamu, naye humpa amtakaye, tena humtawaza juu yake aliye mnyonge. ''…

Kumbuka alilosema Yesu katika Luka 21? 24? Kwamba Yerusalemu utakanyagwa na watu wa Mataifa hadi ukamilifu wa nyakati za watu wa Mataifa!

Kwa vile Zecharia 14? 1-3 inaonyesha kwamba Yesu Kristo atarudi ili aokoe Yerusalemu kutoka kwa Mataifa, ni wazi kwamba KURUDI KWAKE KRISTO MARA YA PILI KUTAFANYIKA KABLA YA NYAKATI ZA MATAIFA KUKAMILIKA! (Isaya 27? 13; 1 Wakorintho 15? 52) (Hoeh H. What are the Times of the Gentiles? Plain Truth, September 1955)

Ilikuwa baada ya miaka 2520 ambapo wazungu wa Marekani wakapanda kwa nguvu. Huo wakati wa miaka 2520 wa Mataifa umekwisha. Mwaka wa 1970, Mwinjilisti Herman Hoeh aliandika makala inayofanana na hiyo?

Biblia yenyewe inatufafanulia muda huo unaojulikana kama mara saba. Ukifungua Ufunuo mlango wa kumi na mbili, na kuilinganisha mstari wa 6 na 14, utapata kwamba neno ''wakati'' katika unabii linamaanisha mwaka. Basi ''mara saba'' linamaanisha ''miaka saba, '' ambapo kila mwaka una miezi kumi na miwili na siku 30 katika kila mwezi. -ama jumla ya siku 2520 (7x12x20)…

Mungu alikuwa akihusika na watu wa Mataifa katika wakati wa Danieli. Mfalme wa Mataifa Nebukadreza alikuwa akitenda dhambi-akiishi kinyume cha sheria za Mungu. Alikuwa akiwaongoza watu kwenye njia ya mateka ya ulimwengu na kuwafanya watumwa mataifa mengine na watu. Alikuwa akisafiri kwenye njia za vita, siyo ya amani.

Mungu alituma onyo lake. Mfalme hakulitii. Kwa hivyo Mungu alihukumu taifa hilo miaka saba (569-562 K. K) kwa kumlaani Mfalme Nebukadreza kuwa mwendawazimu –hadi akafikiri na kukaa kama mnyama wa mwituni!

Adhabu kama hiyo haijawai kutokea kwa mfalme ye yote! Hakuna taifa ambalo limelaaniwa hivyo!

Baada ya miaka hiyo saba, akili ya Nebukadreza ilirudi kuwa timamu. Basi akatubu, na kukubali kwamba njia zake zilikuwa mbaya, na akaandikia watu hati ya kukubali mbele ya mataifa yote kilichompata yeye na watu wake!

Baada ya miaka hiyo saba ya adhabu, ufalme wa Babeli ulipewa moyo wa mwanadamu. Viongozi wakaanza kufikiria njia za amani badala ya vita. Tazama Danieli 7? 4. Ufalme wa Kaldayo (au Babeli)-unaonyeshwa hapa kwa mfano wa simba mkali-aliyesimama ''juu kwa miguu miwili kama mwanadamu; naye akapewa moyo wa kibinadamu. ''

Tazama ulinganisho huo. Mfalme Nebukadreza, kwa sababu ya dhambi zake, aliadhibiwa miaka saba mfululizo. Baada ya miaka hiyo saba akawa tena na akili timamu na mara ya kwanza katika maisha yake, akapata kutubu na kuziacha njia za vita huku akizifuata njia za amani…Kama vile alitesa Israeli na Yuda kwa miaka saba ya ''kinabii''-miaka 2520-basi adhabu ya watu wa Mataifa itakuwa hivyo!Mungu alianza kuadhibu taifa hilo kwa kumlaani mfalme wake kwa miaka saba mfululizo. (Hoeh H. There is a Way of Escape. Plain Truth, 1970)

Cha ajabu ni kwamba kuna siku 2520 katika miaka 7 inayobeba siku 360 kwa kila mwaka. Kwa hivyo, hiyo pia inaonyesha wakati ambapo miaka saba ya ''mpango wa amani'' ya Danieli 9? 27 utathibitishwa. ''Maandiko yatakuwa kwenye ukuta'' wakati mpango

huo wa amani utathibitishwa kwa sababu utakuwa mwanzo wa kuhesabu  miaka hadi wakati Dhiki Kuu itakapoanza. Itapita miaka 3 1/2 baada ya mpango huo kuthibitishwa. Na baada ya muda mfupi tutaona ''chukizo la uharibifu, lile lililonenwa na nabii Danieli, limesimama katika patakatifu'' (Mathayo 24? 15).

Wakati haufai kupuzia kwamba Dhiki Kuu inakuja, mtu asiamini kwamba itakuja kabla ya wakati ufaao. Haiwezi kuanza mwaka wa 2019 kwa sababu kuna matukio mengi ambayo yanatakikana kufanyika (Danieli 9? 27; Mathayo 24? 6-15). Na kwa wakati huu twaona kwamba mwaka wa 2022 ndio kuna uwezekano wa mwanzo wa mambo haya (tutajua mwaka huo baada ya kuona thibitisho la mpango huo wa amani wa Danieli 9? 27).

Mara baada ya Dhiki Kuu kuanza, kutakuwako na miezi arobaini ambayo watu wa Mataifa ''kwa maana Mataifa wamepewa hiyo, nao wataukanyaga mji mtakatifu miezi arobaini na miwili'' yaani Yerusalemu (Ufunuo 11? 2).

## Kuna Habari Njema

Baada ya miaka saba kuisha, Yesu, Mfalme wa Amani (Isaya 9? 6), atarudi na kuziharibu nguvu za watu wa Mataifa zilizokuwa zikitawala ambao pia wataungana kumpiga vita (Ufunuo 19? 19-21).

Tazama pia yafuatayo ambayo yanaonyesha kwamba mabakio wa Israeli watafedheheka, kwa wakati, na watu wa Mataifa lakini Bwana atakuja?

> 25 Nami nitafanya agano la amani nao, nami nitawakomesha wanyama wakali kati yao; nao watakaa salama jangwani, na kulala msituni. 26 Nami nitawafanya wao, na mahali palipo pande zote za mlima wangu, kuwa baraka, nami nitaleta manyunyu kwa wakati wake; yatakuwa manyunyu ya baraka. 27 Na mti wa kondeni utazaa matunda yake, nayo ardhi itatoa mazao yake, nao watakuwa salama katika nchi yao; nao watajua ya kuwa mimi ndimi BWANA, nitakapovunja vifungo vya kongwa lao, na kuwaokoa katika mikono ya watu wale waliowatumikisha. 28 Hawatakuwa mateka ya makafiri tena, wala mnyama wa nchi hatawala; bali watakaa salama salimini, wala hapana mtu atakayewatia hofu. 29 Nami nitawainulia miche iwe sifa njema, wala hawataangamizwa kwa njaa katika nchi yao tena, wala hawatachukua tena aibu ya makafiri. 30 Nao watajua ya kuwa wao, nyumba ya Israeli, ni watu wangu, asema Bwana MUNGU. '' (Ezekieli 34? 25-30)

> 7 Kwa hiyo, angalia, siku zinakuja, asema BWANA, ambapo hawatasema tena, Aishivyo BWANA, aliyewatoa wana wa Israeli katika nchi ya Misri; 8 lakini Aishivyo BWANA, aliyewapandisha na kuwaongoza wazao wa nyumba ya Israeli kutoka nchi ya Kaskazini, na kutoka nchi zote nilikowafukuza; nao watakaa katika nchi yao wenyewe . (Yeremia 23? 7-8)

Wakati wa utawala wa Mataifa umetabiriwa (Ezekieli 7? 24. 30? 1-3, 34? 25-30; Yeremia 10? 25; Luka 21? 23-24; Ufunuo 11? 2), lakini utakuja kuisha. Kanisa la Mungu la awali wa WCG lilifundisha?

> Kwa kurudi kwa Yesu mara ya pili,  ''wakati wa Mataifa'' hatimaye utakuja kuisha. (Stump K. The Arab World in Prophecy. Plain Truth, December 1979, p. 38)

Yesu atasimamisha Ufalme wa Mungu wa miaka elfu! Hiyo ndiyo habari njema.

## Dhiki Kuu Inaanza Kabla ya Danieli 11:40

Inafaa tujue kwamba makundi mengine ya Laodikia wanafundisha mpangilio usiofaa wa unabii kwamba Mfalme wa Kaskazini atavamia Mfalme wa Kusini, ndiposa wakati wa Taabu ya Yakobo utaanza na Dhiki Kuu na Marekani na/hata Uingereza watashambuliwa.

Hii ni dhana mbovu na siyo ya kimantiki kwa sababu nyingi.

Kwanza, shambulizi dhidi ya mashirikisho ya mataifa katika Mashariki ya Kati na Afrika Kaskazini (ambayo ndiyo Mfalme wa Kusini atatawala), halitakuwa sehemu ya TAABU YA YAKOBO.

Ya pili, mataifa yanayotajwa katika mafungu hayo ya Mfalme wa Kusini (Danieli 11? 40-43) siyo Marekani au Uingereza ama wazungu wengine wenzao. Na kwa sababu 'Siku ya Bwana' itakuwa mwaka mmoja na utakuja baada ya Dhiki Kuu, Danieli 11? 44-45 lazima

ije kuelekea MWISHO wa Siku ya Bwana.

Katika mpangilio wa Danieli 11, Dhiki Kuu itaanza katika mstari wa 39, sio Mstari wa 40.

Wacha tuangalie Danieli 11 tukianza na mastari wa 40?

> 40 na wakati wa mwisho mfalme wa kusini atashindana naye; na mfalme wa kaskazini atamshambulia kama upepo wa kisulisuli, pamoja na magari ya vita, na wapanda farasi, na merikebu nyingi; naye ataingia katika nchi hizo, na kufurika na kupita katikati. 41 Tena ataingia katika hiyo nchi ya uzuri, na nchi nyingi zitapinduliwa; lakini nchi hizi zitaokolewa na mkono wake, Edomu, na Moabu; na wakuu wa watu wa Amoni. 42 Naye ataunyosha mkono wake juu ya nchi hizo hata na nchi ya Misri haitaokoka. 43 Lakini atakuwa na nguvu juu ya hazina za dhahabu na fedha, na juu ya vitu vyote vya Misri vyenye thamani; na Walibia na Wakushi watafuata nyayo zake. (Danieli 11? 40-43)

Mafungu haya yanaonyesha kwamba mamlaka katika Mashariki ya Kati na Afrika Kaskazini (ambapo sasa inatawaliwa na Uislamu) zitashindwa. Wengine wanaonekana kuamini kwamba 'wakati wa mwisho' hautaanza kabla ya mstari wa 40, lakini hiyo ni kukosa kuelewa jinsi nakala ya Kiebrania zinafaa zieleweke. Neno ''na'' lia linalopatikana katika mstari wa 40 sio mwanzo wa wakati ule wa mwisho, lakini ni mwendelezo wa kile kilichoanza katika mstari wa 39 wa Danieli 11. Hii inajulikana na wengine.

Kwa mfano, maandishi ya Barne kuhusu Biblia inasema?

Wakati wa mwisho...''Wakati wa mwisho ''unafaa uashirie ukamilisho wa mafuatano wa matukio kwa kuzingatia masuala na kwa mwisho wa shughuli ambazo zimetajwa katika sehemu ya awali ya njozi hiyo ya Danieli. Ni sawa na kile ambacho tunapaswa kusema na kueleza kama? ''kukamilisha jambo. ''

Njia PEKE ya kupatanisha kwamba wakati wa taabu ya Yakobo (Yeremia 30? 7) unaanza na mwanzo wa Dhiki Kuu (Mathayo 24? 21) ni kugundua kwamba itaanza na Mstari wa 39 wa mpangilio katika Danieli 11. Wale wanaoamini kuwa Dhiki Kuu inaanza BAADA ya Mfalme wa Kaskazini kushambulia Mfalme wa Kusini hawatatambua unabii hadi itakapochelewa.

## Wakristo Wengine Watalindwa Wakati wa Dhiki Kuu, Wengine watateswa

Twapaswa tujue kwamba Yesu pia aliuita wakati huu kuwa wakati wa jaribio na aliahidi kuwalinda sehemu ya Wanafiladelfia wa Kanisa la Mungu kutoka kwa Dhiki hiyo?

> 7 Na kwa malaika wa kanisa lililoko Filadelfia andika? Haya ndiyo anenayo yeye aliye mtakatifu, aliye wa kweli, aliye na ufunguo wa Daudi, yeye mwenye kufungua wala hapana afungaye, naye afunga wala hapana afunguaye. 8 Nayajua matendo yako. Tazama, nimekupa mlango uliofunguliwa mbele yako, ambao hapana awezaye kuufunga, kwa kuwa unazo nguvu kidogo, nawe umelitunza neno langu, wala hukulikana jina langu. 9 Tazama, nakupa walio wa sinagogi la Shetani, wasemao kwamba ni Wayahudi, nao sio, bali wasema uongo, Tazama, nitawafanya waje kusujudu mbele ya miguu yako, na kujua ya kuwa nimekupenda. 10 Kwa kuwa umelishika neno la subira yangu, mimi nami nitakulinda, utoke katika saa ya kuharibiwa iliyo tayari kuujiliwa ulimwengu wote, kuwajaribu wakaao juu ya nchi. 11 Naja upesi. Shika sana ulicho nacho, asije mtu akakitwaa taji yako. (Ufunuo 3? 7-11)

Biblia pia ni wazi kwamba wale watakaolindwa 'watakusanyika pamoja' (Sefania 2? 1-3).

Na wakati wengine wanaamini kimakosa kwamba Ufunuo 3? 10 inaonyesha unyakuzi wa Wakristo wote kabla ya dhiki, huo SIO ukweli ambao Yesu amenena. Biblia ni wazi kwamba sehemu kubwa ya kanisa itapitia mateso na dhiki kwa muda wa miaka 3 1/2 ?

> 17 Joka akamkasirikia yule mwanamke, akaenda zake afanye vita juu ya wazao wake waliosalia, wazishikao amri za Mungu, na kuwa na ushuhuda wa Yesu (Ufunuo 12? 17).

Ni kwa sababu ya auminifu na ustahimilivu wao ndio maana Wanafiladelfia wameahidiwa ulinzi kutoka kwa Dhiki Kuu.

Yesu, hata hivyo, anawarudi Kanisa la Laodikia,

ambalo linasimamia Wakristo wengi katika wakati wa mwisho wa kipindi cha kanisa, kwa sababu ya roho yao yenye uvuguvugu. Kukosa imani ya kutosha katika juhudi, Laodikia wamekabiliwa na ulegevu wa mambo ya ulimwengu, bila kujua kwamba ni maskini kiroho, wako uchi na wanahitaji toba (Ufunuo 3? 14-18).

Kwa sababu ya tabia yao, Yesu atawatabisha Walaodikia nje ya kinywa chake na atawaacha waingie katika Dhiki Kuu.

Hii ni kuwaamsha na kuwaleta wajisalimishe kabisa chini yake. Kuelewa tofauti ilioko kati ya zamu la kanisa la mwisho linaturuhusu kuelewa unabii katika Ufunuo 12 ambao unaeleza jaribio la Shetani kutaka kufanya vita na ''mwanamke''-yaani kanisa la kweli.

Makanisa ya Mungu la Laodikia wana upotofu mwingi wa kiunabii kiasi kwamba wasipotubu hawatajua wakati Dhiki Kuu itatokea hadi itakapochelewa sana-nimeandika makosa mengi ya kiunabii ambayo yanafundishwa na Walaodikia (cf. http? //www. cogwriter. com/laodicdeanchurch. htm).

Inafaa tukumbuke kwamba Yesu alifundisha kuwa Wanafiladelfia (Ufunuo 3? 7-13) watalindwa kutoka kwa 'wakati wa mateso' (Ufunuo 3? 10), lakini hakuwaahidi Walaodikia ulinzi (Ufunuo 3? 14-22); kwa sababu ya vipaumbele ambavyo havistahili na mafundisho ya kiunabii ambayo ni ya uwongo, Laodikia lazima watapitia Dhiki Kuu. Biblia ni wazi kwamba kuna Wakristo wa ukweli ambao watapitia Dhiki Kuu kwa muda wa miaka 3 1/2 ya Dhiki Kuu na Siku ya Bwana (Danieli 12? 17; Danieli 7? 25).

Kumbuka pia aliloandika Danieli kuhusu mateso yanayokuja ambayo mfalme wa Mnyama atatumia wakati huo?

> 24 Na habari za zile pembe kumi, katika ufalme huo wataondoka wafalme kumi; na mwingine ataondoka baada ya hao; naye atakuwa mbali na hao wa kwanza; naye atawashusha wafalme watatu. 25 Naye atanena maneno kinyume chake Aliye juu, naye atawadhoofisha watakatifu wake Aliye juu; naye ataazimu kubadili majira na sheria; nao watatiwa mikononi mwake kwa wakati, na nyakati mbili, na nusu wakati. (Danieli 7? 24-25).

Kuna nyakati mbili ya mateso katika mafungu haya. Wakati wa kwanza ni ule ambao Mnyama ''atadhoofisha watakatifu wa Mungu Aliye juu, '' na kwa muda mchache baadaye ''watakatifu wa Aliye juu watatiwa mikononi mwake'' kwa muda wa miaka 3 1/2 (wakati mmoja 1+nyakati mbili 2+nusu wakati 1/2 =ni sawa na miaka 31/2 ). Huyu mfalme wa mnyama anayedhoofisha ndiye Mfalme wa Kaskazini wa mwisho wa Ulaya. Wakristo waliteswa katika nyakati zilizopita, na bado watateswa katika nyakati za mwisho.

Lakini je, watu wengine watakuwaje, wale ambao sio Wakristo?

Pamoja na maonyo yatakayotolewa na mashahidi wawili kwa miaka 3 1/2 (Ufunuo 11? 3), Mungu atalitoa onyo la toba kwa njia ya malaika watatu?

> 6 Kisha nikaona malaika mwingine, akiruka katikati ya mbingu, mwenye Injili ya milele, awahubiri hao wakaao juu ya nchi, na kila taifa, na kabila na lugha na jamaa, 7 akasema kwa sauti kuu, Mcheni Mungu, na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu yake imekuja. Msujudie yeye aliyezifanya mbingu na nchi na bahari na chemchemi za maji. 8 Kisha mwingine, malaika wa pili, akafuata akisema, Umeanguka, umeanguka Babeli, mji ule ulio mkubwa, maana ndio uliowanywesha mataifa yote mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake. 9 Na mwingine, malaika wa tatu, akawafuata, akisema kwa sauti kuu, Mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa yake katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake, 10 yeye naye atakunywa katika mvinyo wa ghadhabu ya Mungu iliyotengenezwa, pasipo kuchanganywa na maji, katika kikombe cha hasira yake; naye atateswa kwa moto na kiberiti mbele ya malaika watakatifu, na mbele za Mwana-Kondoo. 11 Na moshi wa maumivu yao hupanda juu hata milele na milele, wala hawana raha mchana wala usiku, hao wamsujuduo huyo mnyama na sanamu yake, na kila aipokeaye chapa ya jina lake (Ufunuo 14? 6-11).

Mungu anataka kila mtu mahali popote watubu(Matendo 17? 30) na hata kama wengi hawatasikia wito huo kwa wakati huu, bado anataka waonywe (na umati wa watu watasikia kulingana na Ufunuo 7? 8-10).

Wakati wa mwisho wa Mataifa ni pamoja na Siku ya Bwana?

> 2 Mwanadamu, tabiri, useme, Bwana MUNGU asema hivi; Pigeni makelele ya uchungu, Ole wa siku ile! 3 Kwa maana siku ile i karibu, siku ile ya BWANA i karibu, siku ya mawingu; itakuwa wakati wa mataifa. (Ezekieli 30? 2-3)

Tazama unabii wa wakati wa dhiki ya mwisho katika Maandiko ya Kiebrania?

> 29 Lakini huko, kama mkimtafuta BWANA, Mungu wako, utampata, ukimtafuta kwa moyo wako wote, na roho yako yote. 30 Na wakati uwapo katika mashaka, ukiisha kupatwa na mambo haya yote, siku za mwisho, utamrudia BWANA, Mungu wako, na kuisikiza sauti yake; 31 kwa kuwa BWANA, Mungu wako, ni Mungu wa rehema; hatakukosa wala kukuangamiza, wala hatalisahau agano la baba zako alilowaapia. (Kumbukumbu la Torati 4? 29-31)

Kwa hivyo, usaidizi kutoka kwa Mungu wakati huu wa shida utakuwepo tu kwa wale wanaojitahidi kwa ukweli.

Yesu alifundisha?

> 34 Basi, jiangalie, mioyo yenu isije ikalemewa na ulafi, na ulevi, na masumbufu ya maisha haya; siku ile ikawajia ghafula, kama mtego unasavyo; 35 kwa kuwa ndivyo itakavyowajilia watu wote wakaao juu ya uso wa dunia nzima. 36 Basi, kesheni ninyi kila wakati, mkiomba, ili mpate kuokoka katika haya yote yatakavyokea, na kusimama mbele za Mwana wa Adamu. (Luka 21? 34-36)

Unapaswa kuomba na kuchukua hatua ili ulindwe. Hili ndilo Yesu anawaambia Wakristo kufanya.

Ulinzi upo kwa Wakristo Wanafiladelfia.

Miaka 3 1/2 baada ya Dhiki Kuu, Yesu atarudi.

## Mfuatano Mfupi wa Mambo na Habari Njema

Wakati madhumuni ya makala hii yamekuwa juu ya yale ambayo Biblia inafundisha kuhusu vile Dhiki Kuu na wakati wa mwisho wa Mataifa utakuwa, wengi wangependa kujua matukio mengine haswa ya kuangaliwa ambayo yatatokea kabla ya Dhiki Kuu.

Mfuatano wa kimsingi unaanza na ukweli kwamba huzuni na taabu utaendelea (Marko 13? 5-8). Wakati matukio haya yanatokea, taifa lingine litakuwa na deni kubwa (Habakuki 2? 6)-jambo hili litakumba Marekani.

''Mpango wa amani'' wa Danieli 9? 27 utatengenezwa na kuthibitishwa. Huu unaanza hesabu ya miaka hiyo hadi mwisho.

Mfalme wa Kaskazini (ambaye ni mfalme katika Danieli 9? 27) na Mfalme wa Kusini (Danieli 11? 27) watatokea. Ulaya itapata ''jeshi kubwa'' (Danieli 11? 25). Tunaona misingi hiyo ya kuwa na jeshi kubwa ikiwekwa sasa.

Dhabihu ya wanyama zitaanza (Danieli 9? 27). Kumbuka? Kuna uwezekano kwamba Mfalme wa Kusini anaweza kutokea kabla ya Danieli 9? 27 ama baada ya dhabihu kurejeshwa na Mfalme wa Kaskazini na jeshi lake watatokea katika miaka ya ajabu baada ya mpango wa Danieli 9? 27 kuthibitishwa).

Wakati huo Injili itakuwa imehubiriwa ya kutosha kwa ulimwengu kama ushuhuda ili mwisho ufike (Mathayo 24? 14). Jambo hili laonekana kuhusiana na ''kazi itakayomalizika'' ya Warumi 9? 28-maandalizi ya kazi hii pia imeanza wakati sisi katika Kanisa la Mungu Linaloendelea tunatekeleza Mathayo 24? 14 na Warumi 9? 28.

Dhabihu za Kiyahudi zitakomeshwa (Danieli 9? 27). Wayahudi wengine wataamua kuanza kutoa dhabihu ya kila siku, lakini serikali ya Israeli wa kisasa haitakubali.

Nchi ya Ulaya itajipanga tena katika ''falme'' kumi (Sio lazima mataifa kumi yanayokuwepo sasa kama vile wengine wanavyosisitiza) na watampa nguvu Mnyama wa Ufunuo 17? 12-13. Baadhi ya mambo haya yanaweza kufanyika mapema-na kujipanga upya kumependekezwa kufanyika Ulaya.

Chukizo la uharibifu basi litasimamishwa (Mathayo 24? 15; Marko 13? 14) kwa sababu ya hatua za Mfalme wa Kaskazini (Danieli 9? 27; 11? 31). Waaminifu zaidi wanatarajiwa kuendelea kuwaambia watu kinachoendelea hadi watakapokatazwa (Amosi 8? 11-12; Warumi 9? 28).

Amri itatolewa (Sefania 2? 1-3) na baadaye Wanafiladelfia walio waaminifu sana watakimbia kuelekea nyikani (Ufunuo 12? 14-16) na wale walioko Yudea wanapaswa kutoroka kulingana na maelezo ya Yesu katika Mathayo 24? 15-19 na Marko 13? 15-18. Kabla Dhiki Kuu haijaanza, mashahidi wawili watasaidia kufanya kazi, na kwa siku nyingi kabla ya dhiki, watapata nguvu ya kufanya kazi yao ya mwisho (Ufunuo 11? 3-15).

Kwa kusaidiwa na Mpinga Kristo, Dhiki Kuu itaanza (Mathayo 24? 21-22; Marko 13? 19-20; Danieli 11? 39, 12? 1b; Habakuki 2? 7-8).

Hii Dhiki itawamaliza Marekani na mataifa mengine ambao ni halmashauri ya Waingereza (Danieli 11? 39; Yeremia 30? 7; Habakuki 2? 7-8. Mfalme wa Kusini baadaye atasukuma dhidi ya Mfalme wa Kaskazini na ataondolewa pia (Danieli 11? 40-43)-wale walio waaminifu kwa huyo kiongozi wataharibiwa kwa dhiki (Tazama Ezekieli 30? 2-8).

Kwa muda wa mwezi mmoja ama kabla ya miaka 2 1/2 baada ya Dhiki Kuu kuanza, muhuri wa sita utafunguliwa, basi kutakuwepo na ''mwezi kama wa damu'' na jua litakua jeusi (Ufunuo 6? 12; Yoeli 2? 30-31; tazama pia Mwezi wa Damu na Unabii), alafu watu 144, 000 wa Ufunuo watatiwa muhuri.

Muda mfupi baadaye, muhuri wa saba utafunguliwa (Ufunuo 8? 1-6) alafu mwaka mmoja mfululizo wa Bwana (Isaya 34? 8) utaanza na vilio vya baragumu, tauni, n. k. (Ufunuo 8? 7-13; 9? 1-21; 11? 13-14). Kusanyiko la Har-Magedoni litaanza kuhusiana na mlio wa baragumu wa sita (Ufunuo 8? 13-19; 16? 12-16).

Hatimaye Yesu atarudi mara ya pili?

> 28 kadhalika Kristo naye, akiisha kutolewa sadaka mara moja azichukue dhambi za watu wengi, atatokea mara ya pili pasipo dhambi, kwa hao wamtazamiao kwa wokovu. (Waebrania 9? 28)

> 20 Yeye mwenye kuyashuhudia haya asema, Naam; naja upesi. Amina; na uje, Bwana Yesu. (Ufunuo 22? 20)

Na Ufalme wa Mungu utasimamishwa?

> 15 Malaika wa saba akapiga baragumu, pakawa na sauti kuu katika mbingu, zikisema, Ufalme wa dunia umekwisha kuwa ufalme wa Bwana wetu na wa Kristo wake, naye atamiliki hata milele na milele. (Ufunuo 11? 15)

Hiyo ni habari njema!

Usiwe kama wengine ambao wanadhani kwamba Dhiki Kuu haiwezi kuja kwa wakati wao.

Usiwe kama wengine ambao wanadhani kwamba Mungu atawalinda kwa sababu amewapenda. Wakati Mungu amependa kila mmoja, Yesu aliahidi kuwalinda Wanafiladelfia peke yake wakati wa Dhiki Kuu. Wakristo wengi wanaoishi katika siku za Dhiki Kuu hawalindwa (Danieli 7? 25; Ufunuo 13? 5-7).


## Vitabu vya bure zaidi vya Kanisa la Mungu *Linaloendelea*

www. ccog.org/books



Proof Jesus is the Messiah



The Decalogue, Christianity, and the Beast



Should You Keep God's Holy Days or Demonic Holidays?



Where Is The True Christian Church Today?

# Kuitekeleza Mathayo 24:14 Pamoja na Mathayo 28:19-20



*Linaloendelea* Kanisa la Mungu www.ccog.org
Taarifa *za Unabii wa Biblia za kilasiku* www.cogwriter.com

**CCOG.ASIA** Hii ni Tovuti ilengayo wasomaji kutoka Asia.Inazo makala katika lugha ya Kichina cha Mandarin pia na katika Kiingereza pamoja na lugha zingine za Kiasia.
**CCOG.EU** Hii ni Tovuti kwa wale wa Ulaya.Inazo makala katika lugha nyingi za Ulaya.
**CCOG.IN** Hii ni Tovuti inayolenga walio wa asili ya Kihindi.
**CCOG.NZ** Hii ni Tovuti inayolenga walio wa asili ya New Zealand.
**CCOGCanada.CA** Hii ni Tovuti ilengayo walio wa asili ya Canada.
**CDLIDD.ES** Hii ni ya Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG) katika lugha ya Kihispania.
**PNIND.PH** Patuloy na Iglesya ng Diyos. Hii ni Tovuti kwa ajili ya wale wa Ufilipino ama wenye asili yao.

---

***Chaneli ya Habari za Unabii wa Biblia***
*www.youtube.com/BibleNewsProphecy*

***Chaneli ya Kanisa la Mungu Linaloendelea***
*www.youtube.com/continuingcog*

***Chaneli ya utengenezaji wa katuni katika***
*www.youtube.com/ccogafrica*

---

The *Continuing* Church of God pia hutumia majarida pamoja na magazeti ya kielektroniki,vitabu na barua za kila juma kwa waumini wake katika kutekeleza Mathayo 24:14 pamoja na Mathayo 28:19-20.

Swahili Edition